BENKI KUU YA TANZANIA

# UCHUMI WETU

TOLEO NA. 01, JULAI 2025





# KUTOKA MEZA YA GAVANA

**Ndugu Wasomaji,**

Ninayo furaha kubwa kuwakaribisha kusoma toleo la kwanza la jarida la UCHUMI WETU. Jarida hili litakuwa linatoka kila robo mwaka, likiwa ni mojawapo ya nyenzo ambayo Benki Kuu ya Tanzania itaitumia kwa ajili ya kutoa elimu na taarifa mbalimbali kwa umma kuhusu majukumu yetu ya msingi ya kudhibiti mfumuko wa bei, kusimamia mifumo ya malipo, kukuza ujumuishi wa kifedha, ukuaji wa uchumi endelevu na kuhakikisha kuna uthabiti wa sekta ya fedha.

Katika jarida la UCHUMI WETU, mtapata fursa ya kusoma habari zinazotoka Benki Kuu moja kwa moja, sekta binafsi pamoja na sekta nyingine za kiuchumi. Lengo ni kuwawezesha kuelewa mwenendo wa sekta ya fedha kwa ujumla ambayo ni mhimili mkubwa wa maendeleo ya uchumi wa nchi yetu.

Ni wazi kwamba katika miaka ya hivi karibuni, uchumi wa dunia umekumbwa na changamoto nyingi ambazo zimeathiri kasi ya ukuaji wa uchumi karibu katika nchi zote duniani. Changamoto zilizojitokeza na nyingine ambazo bado tunazo hata hivi sasa ni pamoja na kuzuka kwa UVIKO mwishoni mwa mwaka 2019 na kuendelea, vita nchini Ukraine, kubadilika kwa sera za Marekani kulikosababisha kuadimika kwa fedha za kigeni hasa dola ya Marekani pamoja na kuongezeka kwa hatihati za kisiasa Mashariki ya Kati. Mambo yote haya yamesababisha uchumi wa nchi mbalimbali, ikiwemo Tanzania kuguswa na kuhitaji hatua na maamuzi thabiti ili kukabili hali hiyo na kuhakikisha kwamba uchumi unaendelea kukua kama kawaida.

Tanzania tumefanikiwa kukabiliana na mdororo wa uchumi kutokana na hatua mbalimbali ambazo Benki Kuu ya Tanzania kwa kushirikiana na Serikali pamoja na wadau wengine tumekuwa tukizichukua kuhakikisha Tanzania inaendelea kuhimili hali hiyo hata kuweza kushuhudia ukuaji wa uchumi pamoja na kuwa na maendeleo mazuri katika viashiria mbalimbali vya kiuchumi.

Uchumi wa Tanzania Bara na Zanzibar ulikua kwa kasi ya kuridhisha mwaka 2024, ukichangiwa zaidi na uwekezaji unaoendelea kufanywa na Serikali na sekta binafsi. Kwa upande wa Tanzania Bara, uchumi ulikua kwa asilimia 5.5, ikilinganishwa na 5.1 mwaka 2023. Ukuaji huo ulichangiwa zaidi na shughuli za kilimo, ujenzi, fedha na bima, pamoja na shughuli za uchimbaji madini na mawe. Kwa upande wa Zanzibar, uchumi ulikua kwa asilimia 7.1 mwaka 2024, chini kidogo ya asilimia 7.4 ya mwaka 2023, kufuatia kukamilika kwa baadhi ya miradi mikubwa ya miundombinu na uwekezaji. Licha ya changamoto za kiuchumi duniani, uchumi uliendelea kuwa imara ukichangiwa zaidi na shughuli za malazi na huduma za chakula, hususan kutokana na kuongezeka kwa shughuli za utalii.

Mfumuko wa bei umeendelea kuwa tulivu, ndani ya lengo la nchi na vigezo vya mtangamano wa kiuchumi kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Umoja wa Maendeleo wa Kusini mwa Afrika (SADC). Kwa upande wa Tanzania Bara, mfumuko wa bei ulikuwa wastani wa asilimia 3.1 katika miezi kumi ya kwanza ya mwaka 2024/25, wakati kwa upande wa Zanzibar, ulipungua hadi wastani wa asilimia 5.0, kutoka asilimia 5.9 katika kipindi kama hicho mwaka 2023/24. Hii ilitokana na kupungua kwa bei za mazao pamoja na usimamizi thabiti wa sera ya fedha iliyotekelezwa na Benki Kuu katika kipindi hiko.

Mikopo kwa sekta binafsi, ilikua kwa wastani wa asilimia 15.1 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 18.4 katika kipindi kama hicho mwaka 2023/24. Mwenendo huu unaakisi utekelezaji wa sera ya fedha iliyolenga kudhibiti viashiria vya mfumuko wa bei kutokana na kupungua kwa thamani ya shilingi dhidi ya fedha za kigeni.

Aidha, mwaka 2024, sekta ya kibenki nchini Tanzania ilizidi kuimarika, ikiwa na jumla ya mali zenye thamani ya shilingi trilioni 63.5 na faida halisi iliongezeka hadi shilingi trilioni 2.15, kutokana na ongezeko la mahitaji ya mikopo na uboreshaji wa ukwasi. Kiwango cha mikopo chechefu kilikuwa asilimia 3.3, ambacho ni kiwango cha chini zaidi katika Afrika Mashariki, kikionesha usimamizi madhubuti wa vihatarishi na uangalizi makini a shughuli za kibenki. Mafanikio haya yanaonesha mchango mkubwa wa sekta ya benki katika kukuza uchumi.

Ili kukabiliana na shinikizo la mfumuko wa bei duniani, Kamati ya Sera ya Fedha imetangaza kiwango cha Riba ya Benki Kuu cha asilimia 6.0 kwa kipindi cha robo tatu ya mwaka mtawalia kwa lengo la kusawazisha kati ya ukuaji wa uchumi na udhibiti wa mfumuko wa bei.

Benki Kuu inaendelea kusimamia mifumo ya malipo ili kuhakikisha inakuwa salama na yenye ufanisi na tija katika miamala ya ndani na nje ya Tanzania ili kuchochea ukuaji wa uchumi. Vilevile Benki Kuu inandelea kudhibiti kwa karibu watoa huduma ndogo za fedha, kuchagiza matumizi ya huduma rasmi za kifedha, kulinda haki za watumiaji wa huduma za fedha kwa kuanzisha mfumo rahisi wa kutoa malalamiko wa SEMA NA BOT, pamoja na kuweka mazingira wezeshi kwa wabunifu wa huduma za kifedha kuweza kufanya majaribio ya uvumbuzi na ubunifu wao. Lengo ni kuhakikisha kwamba Tanzania inafaidika na maendeleo ya teknolojia na kuharakisha matumizi ya mifumo ya kidigitali katika huduma za kifedha ili kuwafikia watu wengi zaidi kwa muda mfupi zaidi na kwa urahisi.

Mwelekeo wa Benki Kuu kwa siku zijazo ni kuendeleza mfumo wa kifedha wa kisasa unaoweza kusaidia Tanzania kufikia na kuvuka hadhi ya nchi ya kipato cha kati. Ushirikiano wetu na wadau wote wa ndani na wa kimataifa utatuwezesha kufikia malengo haya.

Kupitia jarida hili, tutaweza kupata habari na makala mbalimbali zinazoonesha maendeleo ya sekta ya fedha nchini kwa lengo la kuchagiza ukuaji wa uchumi nchini. Karibu mshirikiane nasi kwa kusoma na kuchangia katika jarida letu la UCHUMI WETU.

**Emmanuel Mpawe Tutuba**
Gavana, Benki Kuu ya Tanzania

# KUTOKA MEZA YA MHARIRI MKUU





**Ndugu Wasomaji,**

Karibu kwenye toleo la kwanza la Jarida letu la UCHUMI WETU. Jarida hili limeandaliwa na Idara ya Mawasiliano ya Benki Kuu ya Tanzania, na litakuwa linatoka kila robo ya mwaka.

Kwenye toleo hili tumekuandalia habari na makala mbalimbali zitakazokupa taarifa muhimu kuhusu majukumu ya Benki Kuu na sekta ya fedha kwa ujumla. Nia ni kukuza uelewa wa wananchi kuhusu masuala ya fedha na uchumi, ili kuongeza ushiriki wa wananchi kwenye sekta rasmi ya fedha. Dhamira yetu ni kuendeleza utulivu wa bei, uthabiti wa sekta ya fedha, na ujumuishi wa huduma za kifedha.

Katika toleo letu hili tutapata habari mbalimbali kuhusu utekelezaji wa sera ya fedha, usimamizi wa sekta ya fedha, mifumo ya malipo, pamoja na mfumo wetu mpya wa kukusanya malalamiko ya watumiaji wa huduma za kifedha kutoka taasisi zinazosimamiwa na Benki Kuu unaoitwa SEMA NA BOT na utendaji wa sekta mbalimbali za uchumi. Aidha, tutawafahamisha kuhusu taarifa mbalimbali za mabadiliko ya kisheria na kikanuni yanayolenga kuimarisha uthabiti wa sekta ya fedha. Mtapata habari kuhusu maendeleo ya mageuzi ya kimkakati na ubunifu unaolenga kuongeza ufanisi na uimara wa mfumo wa kifedha nchini pamoja na ushiriki wetu kwenye mikutano mbalimbali ya kitaifa na kimataifa.

Nawatakia usomaji mwema.

**Victoria Msina**
Meneja, Idara ya Mawasiliano
Benki Kuu ya Tanzania.

# RAIS DKT. SAMIA ATOA TUZO MAALUM KWA BoT

Benki Kuu ya Tanzania imepewa tuzo maalum kwa kutambua mchango wake wa kipekee katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Tuzo hiyo imetolewa tarehe 10 Juni 2025 na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, na kukabidhiwa kwa Gavana wa BoT, Bw. Emmanuel Tutuba katika hafla ya kupokea gawio na michango kutoka kwa taasisi na mashirika ya umma na kampuni ambazo Serikali ina hisa, iliyofanyika Ikulu jijini Dar es Salaam.



Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, akikabidhi tuzo maalum kwa Gavana wa BoT, Bw. Emmanuel Tutuba, katika hafla iliyofanyika Ikulu jijini Dar es Salaam tarehe 10 Juni 2025 .




Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, akizungumza jambo kuhusu Benki Kuu katika hafla ya kupokea gawio na michango kutoka kwa taasisi, mashirika ya umma na kampuni ambazo Serikali ina hisa, iliyofanyika Ikulu jijini Dar es Salaam.



# DKT. MWINYI AZUNGUMZIA USIMAMIZI THABITI WA UCHUMI NCHINI






Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, akiwa pamoja na baadhi ya wageni waalikwa wa kundi maalum hafla ya futari iliyoandaliwa na Benki Kuu ya Tanzania na kufanyika katika hoteli ya Madinat Al Bahr, Zanzibar, tarehe 25 Machi 2025.

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi, ameipongeza Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kwa usimamizi thabiti wa uchumi wa Tanzania. Dkt. Mwinyi alitoa pongezi hizo katika hafla ya futari iliyoandaliwa na Benki Kuu ya Tanzania na kufanyika katika hoteli ya Madinat Al Bahr, Zanzibar.

"Naridhika sana na ushauri wa masuala ya uchumi tunaopewa na Benki Kuu na ndio maana uchumi wa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla umekua vizuri huku tukiwa tunadhibiti mfumuko wa bei vyema," alisema Dkt. Mwinyi.

Alihimiza ushirikiano endelevu kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Benki Kuu ya Tanzania ili kuhakikisha maendeleo ya kiuchumi yanaimarika kwa manufaa ya wananchi wote.

Vilevile, ameipongeza Benki Kuu kwa kuendeleza utamaduni wa kuandaa hafla za futari wakati wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani, zinazojumuisha makundi maalum kama wazee, watoto na watu wenye ulemavu.

"Zanzibar tuna utamaduni wa kusaidia jamii, hususani katika kipindi hiki cha Ramadhani kwahiyo nashukuru sana na ninyi Benki Kuu mnao utaratibu huo, tunawapongeza sana," alisema.

Kwa upande wake, Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Bw. Emmanuel Tutuba, alisema kuwa uchumi wa Tanzania umeendelea kuimarika, huku sekta ya fedha ikikua kwa kasi na mfumuko wa bei ukiwa chini ya wastani wa dunia.

"Kwa mwaka jana uchumi wetu umeendelea kukua, ambapo kwa Tanzania Bara umekua wa asilimia 5.4 na Zanzibar asilimia 7.0, alisema.

Alibainisha kuwa Benki Kuu imeendelea kudhibiti mfumuko wa bei, ambapo kwa mwaka 2024, Tanzania ilikuwa nchi ya tatu duniani kwa kuwa na mfumuko mdogo wa bei.

"Kwa Tanzania Bara, mfumuko wa bei ulikuwa asilimia 3.1, huku Zanzibar ukiwa asilimia 4.5, ikilinganishwa na mfumuko wa bei wa dunia wa asilimia 4.7," alieleza.

Aidha, Gavana Tutuba alizungumzia changamoto katika huduma za kifedha na kuhimiza umuhimu wa elimu ya fedha kwa wananchi ili waweze kufanya maamuzi sahihi kuhusu matumizi ya huduma za kifedha.

Benki Kuu imeandaa miongozo ya elimu ya fedha kwa watu walio katika mfumo rasmi wa elimu pamoja na wale walio nje ya mfumo wa elimu, lengo likiwa ni kukuza uelewa wa wananchi kuhusu masuala ya kifedha na kuimarisha ustawi wao wa kiuchumi.



# WAZIRI MKUU: TUTAENDELEA KUDHIBITI UHALIFU WA KIFEDHA



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa, amesema kuwa Tanzania itaendelea kushiriki kikamilifu na kutekeleza matakwa ya kimataifa katika kupambana na kudhibiti uhalifu wa kifedha, ikiwa ni sehemu ya dhamira yake ya kulinda usalama wa mfumo wa kifedha wa taifa.

Akizungumza katika ufunguzi wa mkutano kati ya Ujumbe wa Tanzania na Kikosi Kazi cha Kimataifa cha Kudhibiti Fedha Haramu (FATF), uliofanyika katika ukumbi wa Benki Kuu Dar es Salaam, Waziri Mkuu amesema kuwa Serikali inatambua ukubwa wa changamoto za uhalifu wa kifedha na imejizatiti kuzikabili kwa kutumia viwango vya kimataifa.

"Tanzania imechukua hatua madhubuti za kuimarisha mifumo yake ya kupambana na fedha haramu. Hatua hizo ni pamoja na kuimarisha uwezo wa taasisi zinazohusika kwa kuwapatia watumishi mafunzo, rasilimali na vifaa vinavyohitajika," alisema.

Ameeleza kuwa baada ya tathmini zilizofanywa na taasisi za kikanda na kimataifa za kudhibiti uhalifu wa kifedha mwaka 2021 na 2022, Tanzania imechukua hatua madhubuti za kuimarisha mifumo yake ya kupambana na fedha haramu. Hatua hizo ni pamoja na kuimarisha uwezo wa taasisi zinazohusika kwa kuwapatia watumishi mafunzo, rasilimali na vifaa vinavyohitajika.



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa, akiwasili katika ofisi za Benki Kuu jijini Dar es Salaam kwaajili ya mkutano kati ya Ujumbe wa Tanzania na Kikosi Kazi cha Kimataifa cha Kudhibiti Fedha Haramu (FATF). Kushoto ni Waziri wa Fedha, Dkt. Mwigulu Nchemba, Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Bw. Emmanuel Tutuba na Naibu Gavana, Bi. Sauda Kassim Msemo.

Amesema kuwa Serikali imeyapa kipaumbele maeneo muhimu katika mapambano dhidi ya uhalifu wa kifedha, ikiwemo kufanya marekebisho ya sheria na sera, kutumia takwimu na teknolojia za kisasa, kuimarisha usimamizi katika sekta ya nyumba na ardhi, kujenga uwezo kwa wadau husika, pamoja na kuimarisha udhibiti na usimamizi wa taasisi za kifedha.

Kwa upande wake, Waziri wa Fedha, Dkt. Mwigulu Nchemba, amesema kuwa baada ya Tanzania kupokea Mpango Kazi kutoka FATF, Serikali ilifanya maamuzi ya ngazi ya juu ya kisera na kiutendaji ili kuimarisha juhudi za kupambana na uhalifu wa kifedha nchini.

Naye, Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Bw. Emmanuel Tutuba alisema kuwa hatua mahsusi zimechukuliwa ili kuimarisha usimamizi wa watoa huduma za fedha za kidijitali na kuongeza uwazi katika sekta ya mashirika yasiyo ya kiserikali. Ushirikiano kati ya taasisi mbalimbali na matumizi bora ya takwimu pia vinaimarishwa ili kusaidia mamlaka kugundua na kukabiliana na uhalifu wa kifedha kwa ufanisi zaidi.



Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa, akizungumza katika mkutano kati ya Ujumbe wa Tanzania na Kikosi Kazi cha Kimataifa cha Kudhibiti Fedha Haramu (FATF) uliofanyika Benki Kuu jijini Dar es Salaam tarehe 14 Aprili 2025.

# TANZANIA YAONDOLEWA ORODHA YA NCHI ZENYE MAPUNGUFU KUPAMBANA NA UTAKATISHAJI FEDHA




Tanzania imeondolewa kwenye Orodha ya nchi zenye mapungufu ya kimkakati katika mifumo ya udhibiti utakatishaji fedha haramu, ufadhili wa ugaidi, na ufadhili wa silaha za maangamizi (Grey List).

Uamuzi huo umetangazwa na Rais wa Kikosi Kazi cha Kifedha cha Kimataifa (FATF), Bi Elisa de Anda Madrazois, mwishoni mwa Mkutano Mkuu wa FATF uliofanyika katika Mji wa Strasbourg nchini Ufaransa kuanzia tarehe 10 hadi 13 Juni 2025.

Ikumbukwe kwamba Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliorodheshwa kwenye orodha ya nchi zenye mapungufu ya kimkakati katika mifumo ya udhibiti utakatishaji fedha haramu, ufadhili wa ugaidi na ufadhili wa silaha za maangamizi (Grey list) mnamo mwezi Oktoba, 2022.

Wakizungumza kwa niaba ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati wa Mkutano wa FATF, Ujumbe wa Tanzania, ukiongozwa na Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kitaifa ya Wataalamu ya Kuzuia Utakatishaji Fedha Haramu, Bi. Sauda Msemo na Kamishna wa Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu (FIU) Bw. Majaba Magana, umeihakikishia FATF na mtandao wa kimataifa kuwa Tanzania ina dhamira ya dhati ya kuhakikisha mifumo yake ya udhibiti inabaki kuwa imara.

"Serikali iatendeleza ushirikiano wa kimataifa; na kusimamia maadili ya uwazi, uwajibikaji na utawala bora kwenye mfumo wa kifedha, ambavyo vitachangia kuimarisha usalama wa nchi, kanda, na mtandao mzima wa kifedha kimataifa" alisema Bi. Msemo.

Akizungumzia kuhusu tukio hilo akiwa Dodoma, Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb) aliishukuru Kamati Ndogo ya Kundi la Afrika kwa ushirikiano katika mchakato mzima, Sekretarieti ya FATF na Kikundi cha Kupambana na Utakatishaji Fedha Haramu Mashariki na Kusini mwa Afrika (ESAAMLG) kwa jitihada kubwa zilizoiwezesha nchi kuondolewa katika grey list na kwamba anatambua na kuthamini msaada wa kitaalam na kifedha kutoka kwa washirika wa maendeleo katika jitihada hizo.

"Tunapenda kuuhakikishia Umma na Jumuiya ya Kimataifa kuwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, amedhamiria kuhakikisha kuwa nchi yetu inabakia kuwa salama dhidi ya vitendo vya uhalifu katika mfumo wa kifedha." Alisema Mhe. Dkt. Nchemba.

Kuondolewa kwa Tanzania kwenye orodha ya nchi zenye mapungufu ya kimkakati katika kupambana na utakatishaji fedha (Grey List of FATF) kunatarajiwa kuongeza imani ya wawekezaji, kupunguza mzigo wa uzingatiaji wa masharti kwa taasisi za fedha, na kuimarisha hadhi ya nchi katika jumuiya ya kifedha kimataifa.

# RIBA YA BENKI KUU YAPUNGUA KUTOKA ASILIMIA 6.00 HADI 5.75

Kamati ya Sera ya Fedha ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT) imeshusha kiwango cha Riba ya Benki Kuu (CBR) kutoka asilimia 6 hadi asilimia 5.75 katika robo ya tatu ya mwaka inayoanza Julai hadi Septemba 2025.

Kiwango cha Riba cha Benki Kuu (CBR) ni kiwango kinachowekwa na Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kama rejea katika utekelezaji wa shughuli zake mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kukopesha benki za biashara. Kiwango hiki huathiri riba za mikopo baina ya benki za biashara, ambazo zinapaswa kuwa ndani ya wigo wa ±2.0% ya CBR iliyowekwa.

Akizungumza katika mkutano wa viongozi wa benki na waandishi wa habari, Gavana wa BoT ambaye pia ni Mwenyekiti wa Kamati ya Sera ya Fedha, Bw. Emmanuel Tutuba, amesema uamuzi huu unatokana na mwenendo mzuri wa kuimarika kwa shughuli za kiuchumi na udhibiti wa mfumuko wa bei.

Uamuzi huu unaakisi imani ya Kamati katika mwenendo wa mfumuko wa bei ambao umeendelea kubaki ndani ya wigo wa asilimia 3–5. Hali hii inatokana na utekelezaji madhubuti wa sera za fedha na bajeti, kuanza kwa msimu wa mavuno, pamoja na utulivu wa thamani ya shilingi ya Tanzania". Amesema Gavana Tutuba.

Ameongeza kuwa, Benki Kuu itatekeleza sera ya fedha ili kuhakikisha riba ya mikopo ya siku saba baina ya benki (7-day interbank rate) inabaki ndani ya wigo wa asilimia 3.75 hadi 7.75.



Gavana, Bw. Emmanuel Tutuba akizungumza na waandishi wa habari na viongozi wa mabenki katika mkutano wa kutangaza Riba ya Benki Kuu kwa robo ya 3 ya mwaka. Mkutano huo umefanyika tarehe 3 Julai, 2025 katika ofisi za BoT, jijini Dar es Salaam.

Kuhusu mwenendo wa uchumi wa nchi, Gavana amesema umeendelea kuimarika ukichochewa na uwekezaji mkubwa wa Serikali katika miundombinu na kuongezeka kwa shughuli za sekta binafsi, kutokana na kuimarika kwa mazingira ya ufanyaji biashara.

Aidha, amesisitiza kuwa hatari za misukosuko ya nje kwenye matarajio ya mwenendo wa uchumi ni ndogo, kutokana na muundo wa uchumi wa nchi ambao unategemea sekta mbalimbali za uzalishaji, pamoja na utekelezaji thabiti wa sera na programu zinazochochea ukuaji wa uchumi, ambazo zinatarajiwa kusaidia kuhimili misukosuko hiyo.

Akijibu swali la mwandishi wa habari, Mwenyekiti wa Jumuiya ya Mabenki, Bw. Theobald Sabi, alisema kuwa kupungua kwa CBR kunaweza kuchangia kupunguza viwango vya riba vinavyotozwa na benki za biashara. Hata hivyo, viwango hivyo huathiriwa pia na vigezo vingine kama vile nguvu za soko na tathmini ya vihatarishi inayofanywa kwa mteja kabla ya kumpa mkopo.

Riba ya Benki Kuu kwa robo ya 4 ya mwaka 2025 itatangazwa mwezi Oktoba mwaka huu. Hii ni kulingana na kalenda ya mikutano ya Kamati ya Sera ya Fedha ya mwaka.





# MUHTASARI WA TAARIFA YA KAMATI YA SERA YA FEDHA KWA ROBO YA TATU YA MWAKA 2025

**Riba ya Benki Kuu kwa robo ya tatu ya 2025 imepungua kutoka 6.00% hadi 5.75%**




### UKUAJI WA UCHUMI

**Tanzania Bara:**
Inakadiriwa 5.8% katika robo ya kwanza na 5.5% katika robo ya pili ya 2025.

### NAKISI YA URARI WA MALIPO YA KAWAIDA

**Tanzania Bara:**
ulipungua hadi 2.6% ya Pato la Taifa kwa 2024/25, kutoka 3.7% 2023/24.

**Zanzibar:**
inakadiriwa kuwa na ziada ya dola milioni 611.1 mwaka 2024/25, kutoka ziada ya dola milioni 428.5 mwaka uliopita.

### MIKOPO KWA SEKTA BINAFSI

ilikua kwa wastani wa 16.7 % katika robo ya pili ya 2025.

Mikopo chechefu ilipungua hadi 3.4% Mei 2025, chini ya kiwango kinachohimilika cha 5%.

### MFUMUKO WA BEI

**Tanzania Bara:**
wastani wa 3.2% katika robo ya pili ya mwaka 2025.

**Zanzibar:**
ulipungua hadi 4.2% Mei 2025 kutoka 5.3% Mei 2024.

### AKIBA YA FEDHA ZA KIGENI

imefikia takribani dola bilioni 6, kiwango cha juu kwa kipindi cha hivi karibuni.

### THAMANI YA SHILINGI

Thamani ya shilingi dhidi ya dola ilishuka kidogo kwa 0.2% mwaka ulioishia Juni 2025, ikilinganishwa na 12.5% mwaka jana.

# DKT. NCHEMBA AIPONGEZA BENKI KUU KWA USIMAMIZI MAHIRI WA UCHUMI



Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba, akizungumza katika kikao na Bodi ya Wakurugenzi ya BoT kilichofanyika katika ofisi za Wizara ya Fedha jijini Dodoma.

Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba, ameipongeza Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kwa mchango wake mkubwa katika kusimamia kwa ufanisi uchumi wa taifa na kuchochea ukuaji endelevu wa maendeleo.

Dkt. Nchemba alitoa pongezi hizo tarehe 18 Juni 2025 jijini Dodoma, alipokutana na Bodi ya Wakurugenzi ya BoT, inayoongozwa na Mwenyekiti wake ambaye pia ni Gavana wa Benki Kuu, Bw. Emmanuel Tutuba.

Akizungumza katika kikao hicho, Dkt. Nchemba alisema licha ya changamoto za kiuchumi zinazoikumba dunia, Tanzania imeendelea kustawi kiuchumi, hali ambayo inachangiwa kwa kiasi kikubwa na usimamizi madhubuti na utendaji bora wa Benki Kuu. Alieleza kuwa ufanisi huo umechangia kudhibiti mfumuko wa bei na kuimarisha uthabiti wa kiuchumi.

Aidha, aliipongeza Benki Kuu kwa mafanikio katika kusimamia sekta ya fedha, ikiwa ni pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa kutosha wa fedha za kigeni pamoja na kushughulikia kwa ufanisi malalamiko ya wananchi kuhusu huduma za kifedha, hususan mikopo inayotolewa na taasisi za huduma ndogo za fedha.



Gavana Emmanuel Tutuba, akielezea jambo kwa Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba, katika kikao kilichofanyika katika ofisi za Wizara ya Fedha jijini Dodoma.

Vilevile, Dkt. Nchemba aliipongeza Benki Kuu kwa mchango wake mkubwa katika jitihada za kuiondoa Tanzania kwenye orodha ya nchi zenye mapungufu ya kimkakati katika udhibiti wa utakatishaji fedha haramu na ufadhili wa ugaidi (Grey List), hatua ambayo ni ushahidi wa uimara wa mifumo ya udhibiti wa fedha nchini.

Aliitaka BoT kuendeleza weledi katika utekelezaji wa majukumu yake, huku akiahidi kuwa Wizara ya Fedha itaendelea kushirikiana kwa karibu na Benki Kuu ili kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

Kwa upande wake, Gavana wa BoT, Bw. Emmanuel Tutuba, alieleza kuwa Benki Kuu itaendelea kutekeleza majukumu yake kwa umahiri mkubwa, kwa lengo la kuimarisha uthabiti wa sekta ya fedha, kukuza uchumi na kuchangia ustawi wa taifa kwa ujumla.



# MWENENDO WA MFUMUKO WA BEI NCHINI JUNI 2025

## MFUMUKO WA BEI WA JUMLA

*umeongezeka hadi asilimia 3.3 mwezi Juni 2025, ikilinganishwa na asilimia 3.2 iliyorekodiwa mwezi uliopita.*

Mei 2025 **3.2%**

Juni 2025 **3.3%**

## MFUMUKO WA BEI WA VYAKULA

*umeongezeka hadi asilimia 7.3 mwezi Juni 2025 kutoka asilimia 5.6 mwezi Mei, hali iliyochangiwa zaidi na kuongezeka kwa bei ya unga wa mahindi, samaki wakavu, ulezi na nyama ya ng'ombe.*

Mei 2025 **5.6%**

Juni 2025 **7.3%**

## MFUMUKO WA BEI WA BIDHAA ZISIZO ZA CHAKULA

*umepungua hadi asilimia 1.7, kutoka asilimia 2.1 mwezi uliopita.*

Mei 2025 **2.1%**

Juni 2025 **1.7%**

## MFUMUKO WA BEI KATIKA KUNDI LA NISHATI,MAFUTA NA HUDUMA

*umeshuka hadi asilimia 2.1 mwezi Juni 2025, kutoka asilimia 6.1 mwezi Mei 2025. Kushuka huku kumetokana hasa na kupungua kwa bei ya mkaa, kuni, petroli na mafuta ya taa.*

Mei 2025 **6.1%**

Juni 2025 **2.1%**

## MFUMUKO WA BEI USIOHUSISHA BEI ZA VYAKULA NA NISHATI

*umepungua hadi asilimia 1.9 kutoka asilimia 2.1 mwezi Mei 2025, hali inayoashiria kuendelea kwa kupungua kwa bei za bidhaa zisizo za chakula.*

Mei 2025 **2.1%**

Juni 2025 **1.9%**


*Chanzo: Ofisi ya Takwimu ya Taifa (NBS)*

# MWENENDO WA UWEKEZAJI NCHINI

Mwenenda wa uwekezaji nchini umeendelea kuimarika, ukiashiria jitihada za serikali katika kuhakikisha kunakuwa na mazingira wezeshi ya uwekezaji na biashara, sera madhubuti za bajeti na fedha pamoja na kuendelea kuimarika kwa Shilingi ya Tanzania.

Hali hii imechangia, kwa kiasi kikubwa, uwekezaji kutoka nje na ndani kukua kwa kasi. Aidha, kufuatia mwaka wa kihistoria wa 2024—ambapo miradi 901 ilisajiliwa ikiwa ni idadi kubwa zaidi ya miradi ya uwekezaji iliyosajiliwa tangu kuanzishwa kwa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), kipindi cha Januari – Machi 2025 pia kimeshuhudia ongezeko la asilimia 46.7 la mitaji na kufikia Dola za Marekani milioni 2,164.7 ikilinganishwa na kipindi kama hiki mwaka 2024 . Katika kipindi hiki, sekta zilizoongoza kwa kuvutia mitaji mikubwa zaidi ni uzalishaji, kilimo, nishati na usafirishaji (Kielelezo Na 1.1).

## Kielelezo Na. 1.1: Mitaji katika kipindi cha Januari – Machi





*Chanzo: TIC, 2025*

# MIRADI YA UWEKEZAJI

Katika kipindi cha Januari – Machi 2025, miradi 199 yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 2,164.7 ilisajiliwa na inatarajiwa kutoa ajira mpya 24,444 katika sekta mbalimbali zikiwemo kilimo, nishati na miundombinu. Aidha, sekta ya uzalishaji imeendelea kuvutia miradi mingi zaidi sambamba na jitihada za serikali za kukuza uchumi wa viwanda (Kielelezo Na 1.2).

### Kielelezo Na. 1.2: Idadi ya miradi na ajira katika kipindi cha Januari – Machi




*Chanzo: TIC, 2025*

# TAKWIMU MUHIMU KUHUSU DARAJA LA JP MAGUFULI (KIGONGO BUSISI).


Tarehe 19 Juni, 2025, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, **Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan,** alizindua **Daraja la JP Magufuli.** Daraja hilo lililopo **mkoani Mwanza** linaonesha **azma ya Serikali** katika kuimarisha miundombinu na kukuza **Uchumi wa Nchi**. Zifuatazo ni takwimu mbalimbali kuhusiana na daraja hilo.

### TZS 718 BILIONI

Gharama za **ujenzi wa daraja** la John Pombe Magufuli.

### Miaka 100

Muda Ambao **daraja hilo litadumu** kabla ya kufanyiwa **matengenezo makubwa.**



### MUDA WA KUVUKA

Muda wa **kuvuka daraja** hilo kwa sasa ni **dakika 4** ambapo awali kabla ya ujenzi ilikuwa **saa 1 hadi 3** na kuathiri **shughuli za kiuchumi.**

### MAGARI 12,000

Wastani wa magari ambayo **yanavuka kwa siku** ikilinganishwa na **magari 1,600** kabla ya ujenzi wa daraja hilo, hivyo linachochea **uchumi wa Kanda ya Ziwa.**

### AJIRA 10,000

Zinazotarajiwa kuzalishwa kutokana na matumizi ya daraja la JP Magufuli.

### RAIS SAMIA SULUHU

**75.4%**

Asilimia Ambazo **Rais Samia Suluhu Hassan** Ameliendeleza Daraja Hilo Hadi Kukamilika Baada ya **Kuingia Madarakani.**

### WAFANYAKAZI

**92%**

Waliojenga daraja hilo ni **Watanzania.**



### GEITA NA MWANZA

**80%**

Mikoa ya **Geita na Mwanza** inachangia katika **madini ya dhahabu** yanayouzwa nje ya nchi (exports) hivyo daraja hilo **litaongeza mauzo** hayo kutokana na urahisi wa kusafirisha.

### UREFU WA DARAJA

**Km 3.2**

Urefu wa daraja hilo, ambalo ni la **kwanza kwa urefu Afrika Mashariki** na la **sita kwa Afrika**.

### KANDA YA ZIWA

**12%**

Mikoa ya **Kanda ya Ziwa** ni maarufu kwa **uuzaji wa Samaki nje ya nchi**, daraja hili litaongeza uuzwaji huo kwa asilimia 12.

**Chanzo:** Wizara ya Ujenzi, ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Wizara ya Madini.

# WAZIRI JAFO: TANZANIA YAFIKIA VIWANDA 80,128 MAFANIKIO YA DIPLOMASIA YA UCHUMI YA RAIS SAMIA

Tanzania imefikisha jumla ya viwanda 80,128 hadi sasa, kutoka viwanda 50,000 vilivyokuwepo mwaka 2020, ikiwa ni matokeo ya juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita katika kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji kupitia diplomasia ya uchumi inayoongozwa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Hayo yamesemwa Juni 30, 2025 na Waziri wa Viwanda na Biashara, Dkt. Suleiman Jafo, wakati wa ufunguzi wa Mkutano wa Pili wa Maafisa Biashara, Uwekezaji na Viwanda uliofanyika jijini Morogoro. Mkutano huo umeandaliwa kwa ushirikiano kati ya wizara na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA). "Nawapongeza maafisa biashara wote kwa kazi kubwa mnayoifanya katika halmashauri zenu.

Mafanikio haya ya ongezeko la viwanda zaidi ya 30,000 yasingewezekana bila mchango wenu wa kusimamia kwa karibu maeneo yenu, kushirikiana na BRELA, na kuwa kiunganishi kati ya serikali na wajasiriamali," alisema Dkt. Jafo. Alieleza kuwa sekta ya viwanda na biashara imekuwa sehemu muhimu ya ukuaji wa uchumi wa nchi, ambapo sasa bidhaa nyingi zinazalishwa nchini na nyingine zinasafirishwa kwenda nje ya nchi.

Alitaja bidhaa kama mchele kutoka Morogoro unaouzwa Senegal, mahindi yanayouzwa Uganda, Kenya na South Sudan, na bidhaa za viwandani kama vioo na gypsum zinazouzwa Kenya na Burundi.

Katika sekta ya chuma, Waziri Jafo alisema Tanzania sasa ina viwanda 24 vya kuzalisha nondo, ambapo baadhi ya miradi mikubwa kama ujenzi wa Bwawa la Julius Nyerere (JNHPP) hutumia nondo za ndani pekee, na baadhi ya bidhaa hizo husafirishwa hadi DRC Congo na Burundi. Kwa upande wa sukari, alisema uzalishaji umeongezeka kwa kasi, ambapo viwanda kama Kilombero Sugar vimeongeza uwezo wa uzalishaji kutoka tani 130,000 hadi kufikia zaidi ya tani 270,000 kwa mwaka baada ya upanuzi wa mitambo. Alisema hadi kufikia mwaka 2027, Tanzania itazalisha sukari ya kutosha kuliko mahitaji na kuanza kuuza nje.

"Katika cement, tulikuwa tunaagiza kutoka nje, lakini leo tuna viwanda vingi na uzalishaji umefikia tani milioni 10 kwa mwaka dhidi ya mahitaji ya tani milioni 8. Tuna akiba ya tani milioni 2 tunazouza nje," aliongeza.

Aidha, Dkt. Jafo alisisitiza kuwa mchango wa biashara kwenye Pato la Taifa ni asilimia 4 na wa viwanda ni asilimia 7.3, hivyo bado kuna kazi kubwa ya kufikia angalau asilimia 10 kwa kila sekta. Aliwataka maafisa biashara kujitathmini na kuhakikisha wanatekeleza wajibu wao kwa weledi na ubunifu. "Mkutano huu ni fursa ya kufanya tathmini ya pamoja.

Pia nawakumbusha kusimamia kwa uadilifu biashara zinazopaswa kufanywa na wazawa pekee. Hili ni jambo muhimu kwa ulinzi wa soko la ndani," alisisitiza. Mkutano huo umehudhuriwa na maafisa biashara kutoka mikoa yote, wakuu wa taasisi, na wawakilishi wa sekta binafsi, na umelenga kuboresha utendaji wa maafisa hao katika kuimarisha biashara na uwekezaji nchini.

> **Mafanikio haya ya ongezeko la viwanda zaidi ya 30,000 yasingewezekana bila mchango wenu wa kusimamia kwa karibu maeneo yenu, kushirikiana na BRELA**



# BENKI KUU YASHIRIKI MKUTANO WA MWAKA WA TAWIFA JIJINI DODOMA

Benki Kuu ya Tanzania imeshiriki katika mkutano wa mwaka wa Chama cha Wanawake Katika Sekta ya Fedha (TAWIFA) uliofanyika tarehe 14 Aprili 2025, jijini Dodoma. Mkutano huo uliwakutanisha wanawake kutoka taasisi mbalimbali ndani ya sekta ya fedha nchini, ukilenga kujadili masuala ya usawa wa kijinsia na ustawi wa wanawake katika maendeleo ya kiuchumi.
Mgeni rasmi katika mkutano huo alikuwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mheshimiwa Dkt. Doto Biteko, ambaye aliipongeza TAWIFA kwa kuadhimisha mwaka mmoja tangu kuanzishwa kwake, huku akieleza mafanikio yaliyopatikana katika kipindi hicho kifupi.

"Wanawake nchini Tanzania wana mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi wa Taifa. Takwimu zinaonesha kuwa asilimia 35 ya Pato la Taifa linatokana na juhudi za wanawake, ambao pia wanachangia asilimia 70 ya nguvu kazi katika sekta ya kilimo, hasa katika uzalishaji wa mazao ya chakula." Alisema Dkt. Biteko.

Katika hotuba yake, Dkt. Biteko alieleza kuwa Serikali ya Awamu ya Sita, inayoongozwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imeendelea kuchukua hatua madhubuti katika kuwawezesha wanawake kwa kuondoa vikwazo vinavyowakabili na kuongeza fursa za kiuchumi na kijamii.

Baadhi ya hatua hizo ni pamoja na kuwaamini na kuwapa wanawake nafasi za juu za uongozi na maamuzi, kufanya Mapitio na Tathmini ya Utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Jinsia na Maendeleo ya Wanawake ya mwaka 2000, kuandaa miongozo mbalimbali ikiwemo Mwongozo wa Ulinzi na Usalama wa Wanawake na Vijana Vyuoni uliozinduliwa mwaka 2023 na kutoa fursa nyingine mbalimbali za kifedha na kiuchumi kwa wanawake.

Kwa upande wake, Makamu wa Rais wa TAWIFA ambaye pia ni Meneja Idara ya Huduma Jumuishi za Fedha Benki Kuu ya Tanzania, Bi. Nangi Massawe, alieleza kuwa TAWIFA inalenga kuwa jukwaa la kuwaleta pamoja wanawake katika sekta ya fedha kwa ajili ya kujenga sekta yenye usawa na jumuishi.

"Benki Kuu ya Tanzania imekuwa mstari wa mbele katika kuhamasisha usawa ndani ya sekta ya fedha. Tunaunga mkono jitihada za Mheshimiwa Rais katika kuhakikisha tunafikia usawa wa kijinsia kwa asilimia 50 kwa 50 ifikapo mwaka 2033." Alisema Bi. Massawe.

Mkutano huu ni sehemu ya jitihada za kuimarisha mchango wa wanawake katika maendeleo ya kiuchumi, sambamba na kuendeleza majadiliano kuhusu masuala ya sera, uongozi, na fursa za kifedha kwa wanawake nchini.




Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Mhe. Dkt. Doto Biteko, akizungumza katika mkutano wa mwaka wa Chama cha Wanawake katika Sekta ya Fedha (TAWIFA) uliofanyika tarehe 14 Aprili 2025, jijini Dodoma.








Kamishna Msaidizi, Idara ya Uendelezaji wa Sekta ya Fedha, Wizara ya Fedha, Bi. Dionisia Mjema, akimkabidhi tuzo maalum Meneja Msaidizi kutoka Kurugenzi ya Masoko ya Fedha, Dkt. Anna Lyimo, kwa kuwasilisha mada kwenye mkutano wa mwaka wa Chama cha Wanawake katika Sekta ya Fedha (TAWIFA) uliofanyika tarehe 14 Aprili 2025, jijini Dodoma.

# SERIKALI YASAINI MIKATABA YA UNUNUZI NA USAFISHAJI DHAHABU




Gavana Emmanuel Tutuba, Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba na Waziri wa Madini, Mhe. Anthony Mavunde, wakijadili jambo baada ya hafla ya utiaji saini wa mikataba ya ununuzi na usafishaji dhahabu iliyofanyika jijini Dodoma tarehe 16 Juni 2025.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Benki Kuu ya Tanzania imesaini mikataba ya ununuzi na usafishaji dhahabu na kampuni za uchimbaji madini na Kiwanda cha Usafishaji Dhahabu cha Geita (GGR), hatua itayowezesha Benki Kuu kupata vyanzo vya uhakika katika kufanikisha programu yake ya ununuzi wa dhahabu.

Hafla ya utiaji saini wa mikataba hiyo ilifanyika , tarehe 16 Juni 2025, katika Ukumbi wa Kambarage uliopo Wizara ya Fedha jijini Dodoma, na kushuhudiwa na Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba, pamoja na Waziri wa Madini, Mhe. Antony Mavunde.

Akizungumza katika hafla hiyo, Mhe. Dkt.Nchemba alisema hatua hiyo ni sehemu ya utekelezaji wa Kifungu cha 59 cha Sheria ya Madini ambacho kinawataka wachimbaji wa madini kutenga asilimia 20 ya uzalishaji wao kwa ajili ya kuiuza katika masoko ya ndani ikiwemo kuiuzia Benki Kuu ya Tanzania, ambayo imepewa haki ya kwanza kisheria ya ununuzi wa dhahabu.
"Sambamba na hiyo, hatua hii itaiwezesha Benki Kuu kupata vyanzo vya uhakika katika kufanikisha programu yake ya ununuzi wa dhahabu na itasaidia viwanda vya ndani vya usafishaji wa dhahabu kufikia malengo ya kupata ithibati ya kimataifa ya London Bullion Market Association (LBMA)". Alifafanua Mhe. Dkt. Nchemba.

Alisema kuwa mpango wa ununuzi wa dhahabu ni dhamira ya Serikali inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, katika kuhakikisha nchi inakuwa na akiba ya kutosha ya fedha za kigeni, kuongeza mchango wa madini katika pato la Taifa, pamoja na kuongeza thamani ya madini nchini ili kuhakikisha wananchi wote wananufaika na rasilimali za madini.

"Hadi leo Benki Kuu ya Tanzania, imenunua tani 5 za dhahabu sawa na dola za Marekani milioni 554 na kuvuka malengo yake ya kununua dhahabu yenye thamani ya dola za Marekani milioni 350. Hatua hii ni kubwa na ya kihistoria nchini kwetu, kwa kuwa itatuhakikishia kuwa na dhahabu ya kutosha hapa nchini kwa ajili ya kusafishwa katika viwanda vilivyopo hapa nchini, ili kuipa Benki Kuu ya Tanzania, ambayo imeamua kununua na kutunza dhahabu kama sehemu ya fedha za kigeni", alifafanua Mhe. Dkt. Nchemba.

Alisema tangu kuanza kutekelezwa kwa kanuni hiyo mpya, Benki Kuu imeweza kuongeza kwa kasi kiwango cha dhahabu inayonunua kutoka katika soko la ndani na hivyo matarajio ni kufikia malengo yake ya kununua tani 6 za dhahabu kwa mwaka wa fedha wa 2024/25 ili kutunisha akiba ya fedha za kigeni.

"Nitoe wito wa Serikali kwa wadau wote katika jambo hili kuhakikisha kwamba mkakati huu wa Serikali kununua dhahabu unakuwa endelevu. Lengo ni kwamba kama taifa tunakuwa na akiba ya kutosha ya fedha za kigeni katika dhahabu, kwani kwa muda mrefu sasa imedhihirika kwamba bei ya dhahabu imekuwa ni nzuri na inayozidi kupanda mwaka hadi mwaka", alisema Mhe. Nchemba.

Kwa upande wake, Waziri wa Madini, Mhe. Antony Mavunde alisema sekta hiyo




Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba akizungumza katika hafla ya utiaji saini wa mikataba ya ununuzi na usafishaji dhahabu iliyofanyika jijini Dodoma tarehe 16 Juni 2025.

imeongeza mchango wake kwa pato la Taifa kutoka asilimia 9.0 mwaka 2015 hadi asilimia 10.1 mwaka 2024/25.

Alifafanua kuwa sekta ya madini ilikuwa inachangia kiasi cha Sh. bilioni 162 mwaka mzima katika Mfuko Mkuu wa Serikali lakini baada ya marekebisho ya Sheria kwa sasa inachangia kiasi cha Sh. bilioni 753 wakati lengo ni kufikia sh. trilioni moja, lengo ambalo alisema litafikiwa.

"Hiki ni kiasi kikubwa kuwahi kutokea na hii inatokana na maelekezo ya Mheshimiwa Rais, Dkt.Samia Suluhu Hassan, ambaye anatuongoza vema katika nchi yetu, kuhakikisha madini yanaongezwa thamani na kuchangia katika Uchumi wa nchi yetu,"alisema Mhe. Mavunde.

Awali Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Bw. Emmanuel Tutuba, alibainisha kuwa Benki Kuu ya Tanzania ilianza rasmi Mpango wa Ununuzi wa Dhahabu nchini katika mwaka wa fedha 2022/23 kama sehemu ya utekelezaji wa mikakati ya Taifa ya kupunguza utegemezi wa mikopo ya nje kama chanzo kikuu cha akiba ya fedha za kigeni na hivyo kuongeza uwezo wa nchi kujitegemea kifedha.

"Hadi kufikia tarehe 13 Juni 2025, Benki Kuu imefanikiwa kununua kilo 5,022.85 za dhahabu safi, zenye thamani ya takriban Dola za Kimarekani milioni 554.28, Ikiwa imezidi lengo lake la mwaka la kuongeza akiba ya fedha za kigeni kiasi cha dola za Kimarekani 350 million kwa 2024/25", alifafanua Bw. Tutuba.

Aliongeza kuwa kupitia mpango huo, Benki Kuu imelenga kuongeza kiwango cha dhahabu kinachotumika kama sehemu ya akiba ya fedha za kigeni na kuimarisha uhimilivu wa thamani ya shilingi dhidi ya fedha za kigeni nchini.

Kwa upande wa kampuni za madini zilizosaini mikataba hiyo za Shanta Mining, Buckreef, Geita Gold Mining na Kiwanda cha Usafishaji Dhahabu cha Geita (GGR), zimeishukuru Serikali kwa kuendelea kuimarisha sekta ya madini nchini na kuahidi kuwa mikataba hiyo itafungua fursa zaidi katika sekta ya madini.



Waziri wa Madini, Mhe. Anthony Mavunde, akieleza jambo katika hafla ya utiaji saini wa mikataba ya ununuzi na usafishaji dhahabu iliyofanyika jijini Dodoma tarehe 16 Juni 2025.




Gavana Emmanuel Tutuba na Mmiliki wa kiwanda cha kusafisha Dhahabu cha Geita (GGR), Bi. Sarah Masasi, baada ya utiaji saini wa mkataba wa usafishaji dhahabu katika hafla iliyofanyika jijini Dodoma tarehe 16 Juni 2025.




Gavana Emmanuel Tutuba na Mkurugenzi Mtendaji wa Geita Gold Mining (GGML), Bw. Duan Archery, baada ya utiaji saini wa mkataba wa usafishaji dhahabu katika hafla iliyofanyika jijini Dodoma tarehe 16 Juni 2025.




Gavana Emmanuel Tutuba na Afisa Mkuu wa Uendeshaji wa Shanta Gold Ltd, Bw. Honest Mrema,baada ya utiaji saini wa mkataba wa usafishaji dhahabu katika hafla iliyofanyika jijini Dodoma tarehe 16 Juni 2025.




Gavana Emmanuel Tutuba na Kaimu Meneja Mkuu wa Mgodi wa Buckreef, Bw. Isaka Bisansaba, baada ya utiaji saini wa mkataba wa usafishaji dhahabu katika hafla iliyofanyika jijini Dodoma tarehe 16 Juni 2025.

# SEMA NA BOT: KUSHUGHULIKIA MALALAMIKO YA WATEJA WA HUDUMA ZA FEDHA



Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba, akizindua mfumo wa kushughulikia malalamiko ya watumiaji wa huduma za fedha - SEMA NA BOT katika hafla iliyofanyika Juni 5, 2025, jijini Dodoma. Kulia ni Naibu Katibu Mkuu (Huduma za Hazina), Bi. Jenifa Omolo.

Katika juhudi za kulinda watumiaji wa huduma za fedha dhidi ya manyanyaso ya kifedha na kuhakikisha haki na usawa katika sekta ya fedha, Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba, amezindua mfumo mpya wa kushughulikia malalamiko ya wateja uitwao SEMA NA BOT pamoja na muongozo wa Mazingira ya Majaribio ya Teknolojia ya Fedha, katika hafla iliyofanyika Juni 5, 2025, jijini Dodoma.

Katika uzinduzi huo, Dk. Mwigulu amesema mfumo wa SEMA NA BOT utakuwa suluhisho kwa changamoto nyingi zinazowakumba wananchi, hususan wale waliokuwa wakinyanyaswa na taasisi zisizo rasmi za mikopo maarufu kama mikopo umiza au kausha damu. Amesema mikopo hiyo imekuwa chanzo cha mateso kwa wananchi wanaotafuta mikopo ya haraka huku wakikwepa taasisi rasmi za kifedha.

"Kuzinduliwa kwa mfumo wa SEMA NA BOT kutaongeza imani ya umma katika kutumia huduma rasmi za fedha na kuboresha uwajibikaji kwa watoa huduma za fedha wanaosimamiwa na Benki Kuu,"alisema.

Dkt. Nchemba ameipongeza Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kwa kuandaa mfumo unaojibu moja kwa moja changamoto zilizokuwa zikiwakabili wananchi, na kuutaja kama utekelezaji wa dhahiri wa falsafa ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ya 4R kwa kuleta mageuzi katika huduma za fedha.

Kwa upande wake, Gavana wa BoT, Bw. Emmanuel Tutuba, amesema mfumo wa SEMA NA BOT ni wa kidigitali na utamuwezesha mtumiaji wa huduma za fedha kuwasilisha malalamiko kwa njia ya tovuti, simu janja kupitia programu tumishi (Apps), na hata kwa simu za kawaida kupitia USSD.

Aidha, Gavana Tutuba amesema kuwa mfumo huo utawezesha taasisi za fedha kubaini na kushughulikia malalamiko ya wateja kwa haraka, pamoja na kukusanya takwimu za malalamiko yaliyowasilishwa na kushughulikiwa. Takwimu hizo zitatumika kama nyenzo muhimu kwa taasisi za fedha katika kuboresha huduma zao na kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa wateja.

Katika hatua nyingine, Benki Kuu kupitia Wizara ya Fedha imezindua muongozo wa Mazingira ya Majaribio ya Teknolojia ya Huduma za Fedha (Fintech Regulatory Sandbox) kwa lengo la kutoa fursa kwa wabunifu kujaribisha bidhaa na huduma mpya za kifedha chini ya usimamizi wa karibu wa Benki Kuu.

Dkt. Mwigulu alisema kuwa hatua hiyo itaongeza kasi ya ubunifu na kuchochea matumizi ya teknolojia kama vile blockchain, Akili Unde, huduma za malipo kidigitali, mabenki mtandao, ubadilishaji fedha za kigeni na hata uwekezaji kwenye sarafu mtandao (cryptocurrency).

"Teknolojia ya fedha ni kichocheo kikubwa cha ukuaji wa sekta ya fedha na uchumi kwa ujumla. Ni wazi kuwa Tanzania ipo kwenye njia sahihi ya kujenga uchumi shindani, jumuishi na wa kisasa," alisema.

Kwa mujibu wa BoT, tangu kuanza kwa mazingira hayo ya majaribio tarehe 2 Januari 2025, kampuni 62 tayari zimejisajili kuwasilisha maombi ya majaribio ya bunifu mbalimbali.

Naibu Gavana wa BoT (Uthabiti wa Sekta ya Fedha), Bi. Sauda Msemo, amesema kuwa mfumo wa SEMA NA BOT pamoja na Mazingira ya Majaribio ya Teknolojia ya Fedha ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Taifa wa Huduma Jumuishi za Fedha (2023–2028) na Mpango Kabambe wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha (2020/21–2029/30).

Kwa pamoja, jitihada hizi zinatarajiwa kuongeza upatikanaji wa huduma bora, salama, zenye gharama nafuu na zinazowalenga Watanzania wengi zaidi, hasa waliopo maeneo ya vijijini na waliokuwa wakitengwa kwenye mfumo rasmi wa kifedha.




Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba, pamoja na viongozi wa Benki Kuu ya Tanzania waliohudhuria uzinduzi wa mfumo wa kushughulikia malalamiko ya watumiaji wa huduma za fedha - SEMA NA BOT katika hafla iliyofanyika Juni 5, 2025, jijini Dodoma.

# BOT KUSAIDIA WABUNIFU WA TEKNOLOJIA ZA FEDHA NCHINI



Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Bw. Emmanuel Tutuba, ameishukuru Serikali kwa jitihada na mageuzi makubwa ambayo yanasaidia wananchi kupata na kutumia huduma rasmi za fedha zenye ubora wa hali ya juu.

Amezungumza hayo katika hafla ya Uzinduzi wa Mazingira ya Majaribio ya Teknolojia ya Fedha na Mfumo wa Kushughulikia Malalamiko ya Watumiaji wa Huduma za Fedha wa SEMA NA BOT jijini Dodoma tarehe 5 Juni 2025 uliofanywa na Waziri wa Fedha, Dkt. Mwigulu Nchemba.

"Sote tumeshuhudia mageuzi mbalimbali katika sekta ya fedha, yote yakiwa na lengo la kukuza uchumi jumuishi na endelevu," amesema Gavana Tutuba na kutaja hatua hizo kuwa ni pamoja na kutunga sera, sheria na kanuni kwa ajili ya sekta ya benki, watoa huduma ndogo za fedha, bima, pensheni, masoko ya mitaji na mifumo ya malipo.

Licha ya juhudi nzuri za kuongeza upatikanaji na matumizi ya huduma rasmi za fedha, Gavana Tutuba amesema changamoto bado zipo. Amezitaja changamoto hizo kuwa ni pamoja na kutokuwa na mazingira rafiki kwa ukuaji wa teknolojia na ubunifu katika mfumo wa utoaji wa huduma rasmi za fedha na idadi kubwa ya watoa huduma wasio rasmi.

Nyingine ni kiwango cha chini cha elimu ya fedha, uhusiano hafifu baina ya watoa huduma rasmi za fedha na watumiaji, mfumo wa analojia wa kushughulikia malalamiko ya watumiaji wa huduma rasmi za fedha, gharama kubwa za matumizi ya huduma za fedha na ufahamu mdogo wa matumizi ya vifaa vya kidijitali.

Kukabiliana na changamoto hizo, Benki Kuu ya Tanzania, kupitia Baraza la Taifa la Huduma Jumuishi za Fedha, imechukua hatua mbalimbali zikiwemo kuweka Mazingira ya Majaribio ya Teknolojia ya Fedha (Bank of Tanzania Fintech Regulatory Sandbox).

"Mazingira ya majaribio ya Teknolojia ya Fedha yanatoa mazingira wezeshi kwa wabunifu kujaribisha teknolojia za fedha chini ya usimamizi na udhibiti wa Benki Kuu ya Tanzania," amesema Gavana Tutuba.

Ameongeza kwamba mazingira hayo yataifanya Tanzania kuwa miongoni mwa nchi zinazofanya vizuri katika ukuaji wa Teknolojia za Fedha (FinTech), uwajibikaji, na kuchochea matumizi ya huduma jumuishi za fedha zenye ubora, salama na kwa gharama nafuu.

Gavana ameeleza kuwa mazingira ya majaribio ya teknolojia ya fedha yameanza kazi tarehe 02 Januari 2025 ambapo hadi hivi sasa kampuni 62 zimejisajili katika mfumo wa kutuma maombi ya mazingira ya teknolojia ya fedha.

"Maombi haya yalilenga bunifu zinazotumia teknolojia mbalimbali ikiwemo akili mnemba (artificial intelligence); teknolojia ya blockchain katika kutoa huduma mbalimbali za fedha kama vile huduma za malipo, na benki mtandao (digital banking).

Ubunifu mwingine ni unaohusu kubadilisha fedha za kigeni, kutuma fedha nje ya nchi, kununua na kuwekeza katika sarafu mtandao (cryptocurrency), utoaji wa mikopo kwa wajasiriamali; na mifumo inayodhibiti utakasishaji wa fedha haramu.

Katika neno lake la ukaribisho, Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (Uthabiti wa Sekta ya Fedha), Bi Sauda Msemo, alieleza matumaini yake kwamba Mazingira ya Majaribio ya Teknolojia ya Fedha na Mfumo wa Kushughulikia malalamiko ya Watumiaji wa Huduma za Fedha wa SEMA NA BOT vitachochea ustawi na ujumuishi wa huduma za fedha.

Utekelezaji wa mambo hayo mawili ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Taifa wa Huduma Jumuishi za Fedha wa mwaka 2023-2028 na Mpango Kabambe wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha (Financial Sector Development Masterplan 2020/21-2029/30).

**SKANI QR CODE KUPATA MFUMO WA SEMA NA BOT**

# GAVANA AONGOZA MAJADILIANO RIPOTI YA UTHABITI WA SEKTA YA FEDHA 2024




**Gavana wa BoT na Mwenyekiti wa Jukwaa la Uthabiti wa Sekta ya Fedha Tanzania, Bw. Emmanuel Tutuba, akizungumza katika kikao cha 12 cha Jukwaa hilo.**

Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania ambaye pia ni Mwenyekiti wa Jukwaa la Uthabiti wa Sekta ya Fedha Tanzania, Bw. Emmanuel Tutuba, ameongoza kikao cha 12 kilichofanyika tarehe 9 Julai, 2025 katika Ofisi za Benki Kuu -Makao Makuu Ndogo, Dar es Salaam.

Jukwaa hilo linajumuisha Mamlaka za Udhibiti na Usimamizi wa Sekta ya Fedha zipatazo 15 zikiwemo Benki Kuu ya Tanzania, Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Wizara ya Fedha (MOF-URT), Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar (PO-FP (RGoZ), Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Ajira Vijana na Wenye Ulemavu (PMO-LYED), Mamlaka ya Usimamizi wa Bima (TIRA), Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana ( CMSA), Mamlaka ya Mawasiliano (TCRA), Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu (FIU), na Bodi ya Bima ya Amana (DIB).

Jukwaa hilo, miongoni mwa masuala mengine, lilijadili Ripoti ya Uthabiti wa Sekta ya Fedha ya mwaka unaoishia Desemba, 2024 inayolenga kutambua vihatarishi vinavyoweza kutokea na kutathmini uthabiti wa mfumo wa fedha dhidi ya misukosuko ya ndani na nje.



**Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Zanzibar, Dkt. Juma Malik Akil, akizungumza katika kikao kilichojadili masuala mbalimbali kuhusu Ripoti ya Uthabiti wa Sekta ya Fedha Tanzania ya Mwaka 2024.**



**Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Dkt. Natu El-maamry Mwamba, akielezea jambo katika kikao cha 12 cha Jukwaa la Uthabiti wa Sekta ya Fedha Tanzania kilichofanyika tarehe 9 Julai, 2025 katika Ofisi ya Benki Kuu jijini Dar es Salaam.**

Lengo kuu la majadiliano hayo ni kuhakikisha kuwa sekta ya fedha inabaki kuwa thabiti, shindani, na yenye mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi wa Taifa.

Aidha, wajumbe walipitia taarifa mbalimbali za utekelezaji zikiwemo mabadiliko ya tabia ya nchi (climate related risks), mwenendo wa viashiria vinavyotumika kupima uthabiti wa kifedha, upimaji wa uhimilivu wa sekta ya fedha (stress testing), uthibiti wa majanga ya sekta ya fedha ( Financial Crisis Preparedness and Management) na Uthibiti wa usalama wa sekta ya fedha dhidi ya ushambulizi wa kimtandao (cyber security in financial sector).

Akizungumza katika kikao hicho, Mwenyekiti wa Jukwaa hilo, Bw. Emmanuel Tutuba, alieleza kuwa nchi imepiga hatua katika kuhakikisha sekta ya fedha inakuwa thabiti ambapo ni matokeo ya ushirikiano wa Mamlaka zote za Udhibiti na Usimamizi wa Sekta ya Fedha.

Mafanikio hayo yanajumuisha Tanzania kuondolewa katika orodha ya nchi zenye mapungufu ya kimkakati ya Utakatishaji Fedha Haramu, Ufadhili wa Ugaidi na Ufadhili wa Silaha za Maangamizi (AML-CFT).

Pia, Tanzania imewekwa katika daraja la B+ katika tathmini ya nchi kukopesheka katika masoko ya fedha ya kimataifa, ikiwa ni maboresho ikilinganishwa na vipindi vilivyopita.




**Naibu Gavana (Uthabiti na Usimamizi wa Sekta ya Fedha), Bi. Sauda Msemo, akifafanua jambo katika kikao cha 12 cha Jukwaa hilo kilichofanyika tarehe 9 Julai, 2025 katika Ofisi ya Benki Kuu jijini Dar es Salaam.**

# TANZANIA YATEKELEZA KWA MAFANIKIO PROGRAMU ZA IMF



Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Bw. Emmanuel Tutuba, ameshiriki katika kikao cha hitimisho la majadiliano kati ya Serikali ya Tanzania na timu ya wataalam kutoka Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF). Kikao hicho kilifanyika tarehe 17 Aprili 2025 katika ofisi za BoT, jijini Dar es Salaam, na kuongozwa na Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba.

Majadiliano hayo yamefanyika kufuatia kukamilika kwa tathmini ya awamu ya tano ya utekelezaji wa Mpango wa 'Extended Credit Facility' (ECF) ambao unahusisha mkopo nafuu kwa ajili ya kuimarisha uchumi wa nchi kupitia sekta za uzalishaji na huduma za jamii. Vilevile, tathmini hiyo ilijumuisha awamu ya pili ya utekelezaji wa Mpango wa Resilience and Sustainability Facility (RSF), unaolenga kuisaidia Tanzania kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Akizungumza katika kikao hicho, Dkt. Nchemba alieleza kuridhishwa na taarifa iliyowasilishwa na Kiongozi wa Ujumbe wa IMF, Bw. Nicolas Blancher. Taarifa hiyo ilionesha kuwa Tanzania imetekeleza kwa mafanikio vigezo vya IMF katika programu zote mbili za ECF na RSF.


Dkt. Nchemba alisisitiza kuwa Serikali itaendelea kusimamia utekelezaji wa programu hizo kwa umakini mkubwa. Alieleza kuwa jumla ya thamani ya programu hizo mbili ni Dola za Kimarekani bilioni 1.832, ambapo kiasi cha Dola bilioni 1.1 kimetengwa kwa ajili ya kuimarisha uchumi kupitia sekta za uzalishaji, na Dola milioni 786 kwa ajili ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Programu hizo zinatarajiwa kutekelezwa katika kipindi cha miaka minne kuanzia mwaka wa fedha 2022/2023 hadi 2025/2026.

Kwa upande wake, Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Emmanuel Tutuba, alieleza kuwa Serikali kupitia Benki Kuu inaendelea kuweka mazingira rafiki kwa biashara, hasa sekta binafsi, kwa kurasimisha shughuli za biashara kupitia mifuko ya udhamini wa mikopo inayosimamiwa na BoT.

Naye, Bw. Nicolas Blancher, alithibitisha kuwa tathmini ya awamu ya tano imeonesha mafanikio makubwa katika utekelezaji wa mpango wa ECF na RSF. Alipendekeza Serikali iendelee kuchukua hatua hatua zaidi katika kuboresha huduma za jamii na mazingira ya biashara na uwekezaji.



**Gavana Emmanuel Tutuba, akizungumza na Kiongozi wa Ujumbe wa IMF, Bw. Nicolas Blancher baada ya kikao cha hitimisho la majadiliano kati ya Serikali ya Tanzania na IMF kilichofanyika tarehe 17 Aprili 2025 katika ofisi za BOT, jijini Dar es Salaam.**



**Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba, Naibu Gavana , Bi. Sauda Msemo, Naibu Gavana Dkt. Yamungu Kayandabila pamoja na Gavana Emmanuel Tutuba, wakizungumza baada ya kikao cha hitimisho la majadiliano kati ya Serikali ya Tanzania na IMF.**

# BOT YAPATA MWAROBAINI WA MIKOPO UMIZA

**Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Bw. Emmanuel Tutuba**, amezitaka Taasisi za Huduma Ndogo za Fedha Daraja la pili kujiunga na taasisi mojawapo kati ya Mwamvuli wa Taasisi Zinazotoa Huduma Ndogo za Fedha (TAMFI) na Umoja wa Taasisi Zinazotoa Huduma Ndogo za Fedha (TAMIU) ifikapo Mwishoni wa mwezi Desemba 2025.

Gavana Tutuba amesema hayo alipozindua Utaratibu wa Utekelezaji wa Hati ya Makubaliano ya Usimamizi Binafsi wa Sekta ya Huduma Ndogo za Fedha, kati ya Benki Kuu, TAMFI na TAMIU iliyofanyika tarehe 1 Julai, 2025 katika ofisi za BoT jijini Dar es Salaam.

"Taasisi zote za Huduma Ndogo za Fedha Daraja la pili zinalazimika kujiunga na chama kimojawapo kati ya TAMFI au TAMIU ndani ya kipindi cha miezi 6 na zoezi hili linatakiwa kuanza kutekelezwa kuanzia leo tarehe 1 Julai hadi mwishoni mwa Desemba 2025. Taasisi ambayo itakuwa haijajisajili kufikia Desemba tutainyang'anya leseni". Amesema Gavana Tutuba.




**GAVANA BOT:** Taasisi ambayo haitajisajili TAMFI au TAMIU itafutwa usajili ifikapo Desemba 2025



Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Bw. Emmanuel Tutuba, akikata utepe kuashiria kuzindua rasmi Utaratibu wa Utekelezaji wa Hati ya Makubaliano ya Usimamizi Binafsi wa Sekta ya Huduma Ndogo za Fedha, kati ya Benki Kuu, TAMFI na TAMIU. Kushoto ni Mwenyekiti wa Bodi ya TAMFI, Bi. Devotha Minzi na kulia ni Mwenyekiti wa Chama cha TAMIU, Bw. Juma Mnanka.

Amesema kuwa lengo la kuwataka watoa huduma hao kujisajili katika vyama hivi ni kuboresha utoaji huduma na kutatua changamoto mbalimbali zinazosababisha madhila kwa walaji wa huduma hizo.

Aidha, Gavana amesema kuwa utaratibu huu wa usimamizi binafsi utahakikisha TAMFI na TAMIU zinasimamia utendaji wa taasisi zinazotoa huduma ndogo za fedha kwa kuzingatia kanuni zilizopo kwa lengo la kutokomeza changamoto mbalimbali katika sekta hiyo ikiwemo Mikopo Umiza.

"TAMFI na TAMIU watakuwa na wajibu wa kusimamia mwenendo wa wanachama wao kwa kuzingatia kanuni bora za kimaadili, kuhamasisha utoaji wa elimu ya fedha kwa wateja, kusimamia na kuratibu mifumo ya kushughulikia malalamiko, Kuweka taratibu za uwajibikaji na uwazi katika utoaji wa huduma, na Kuwezesha utekelezaji wa kanuni na miongozo ya kiserikali," Amesema

Ameongeza kuwa Benki Kuu itaendelea kusimamia sekta hiyo kupitia utekelezaji wa sera, utoaji wa leseni, ulinzi kwa watumiaji wa huduma za fedha, ufuatiliaji wa mwenendo wa jumla wa sekta, na itahakikisha inashirikiana kwa karibu na vyama hivyo ili kuhakikisha kwamba misingi ya makubaliano hayo yanatekelezwa kikamilifu.

Kwa upande wake, Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (Usimamizi wa Sekta ya Fedha), Bi Sauda Msemo, amesema ongezeko la taasisi ndogo za fedha nchini hadi kufikia 2,600 linamchango mkubwa katika kuongeza ujumuishi wa huduma za fedha nchini na kuendelea kuimarisha uthabiti wa sekta ya fedha.

"Benki Kuu inatambua na kuthamini mchango huu, na ndio maana tumeamua kuanzisha utaratibu wa usimamizi binafsi, utaratibu ambao unalenga kuboresha uwajibikaji na uwazi katika sekta ya fedha, kwa lengo la kuendelea kumlinda mtumiaji wa huduma za fedha," Amesema Bi. Msemo katika hotuba iliyosomwa kwa niaba yake na Mkurugenzi wa Usimamizi wa Sekta ya Fedha, Bw. Sadati Musa.

Naye, Mwenyekiti wa Bodi ya TAMFI, Bi. Devotha Minzi pamoja na Mwenyekiti wa Chama cha TAMIU, Bw. Juma Mnanka, wameipongeza Benki Kuu kwa kuja na utaratibu huu na wameahidi wataendeleza ushirikiano ili kuhakikisha sekta hiyo inaimarika.

# BODI YA BOT YATEMBELEA MIRADI YA KIUCHUMI JIJINI DODOMA




Gavana Emmanuel Tutuba, akizungumza wakati wa ziara ya Bodi ya Wakurugenzi ya Benki Kuu ya Tanzania katika mradi wa ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato, jijini Dodoma.




Bodi ya Wakurugenzi ya Benki Kuu ya Tanzania pamoja na wafanyakazi wa Benki Kuu katika mradi wa ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato, jijini Dodoma.



Naibu Gavana, Dkt. Yamungu Kayandabila (kushoto) akijadiliana jambo na Mkurugenzi wa Masuala ya Shirika CETAWICO, Bi. Katherine Mwimbe, wakati wa ziara ya Bodi ya Benki Kuu katika Kiwanda cha kutengeneza mvinyo wa zabibu CETAWICO jijini Dodoma.

Bodi ya Wakurugenzi ya Benki Kuu ya Tanzania, ikiongozwa na Mwenyekiti wake ambaye pia ni Gavana wa Benki Kuu, Bw. Emmanuel Tutuba, ilifanya ziara katika mradi wa ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato, jijini Dodoma.

Ziara hiyo imefanyika tarehe 17 Juni 2025, ambapo Msimamizi wa Mradi, Mhandisi Kedrick Chawe, alieleza kuwa mradi huo unatekelezwa chini ya usimamizi wa TANROADS kwa ufadhili wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB). Ujenzi huo unajumuisha njia ya kuruka na kutua ndege (runway), jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, pamoja na miundombinu mingine muhimu.

Kukamilika kwa uwanja huu kunatarajiwa kuchochea ukuaji wa sekta ya utalii, kuvutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi, kurahisisha usafirishaji wa mizigo, na hivyo kuongeza mapato ya serikali. Aidha, mradi huu utaimarisha hadhi ya Dodoma kama mji mkuu na kuchangia kwa kiasi kikubwa ukuaji wa uchumi wa taifa.

Katika hatua nyingine, Bodi hiyo ilitembelea Kiwanda cha kutengeneza mvinyo wa zabibu cha CETAWICO kilichopo Hombolo, jijini Dodoma, ambako walipokelewa na Mkurugenzi wa Masuala ya Shirika, Bi. Katherine Mwimbe. Alieleza kuwa uwepo wa kiwanda hicho umeleta manufaa makubwa ya kiuchumi na kijamii, ikiwemo kuongeza kipato cha wakulima wadogo kwa kununua zabibu zao na kutoa ajira kwa zaidi ya watu 5,000 katika sekta ya kilimo kupitia zao la zabibu.

Kiwanda cha CETAWICO kinachangia kutangaza bidhaa za Tanzania katika soko la kimataifa kupitia mauzo ya mvinyo bora, hivyo kuimarisha mnyororo wa thamani wa kilimo na kuchochea maendeleo ya viwanda nchini.

Ziara hizo za Bodi ya Wakurugenzi ya Benki Kuu ya Tanzania katika miradi ya kimkakati na shughuli za kiuchumi zinawawezesha kupata uelewa wa kina kuhusu utekelezaji wa miradi hiyo, changamoto zilizopo, na mchango wake katika kukuza uchumi wa taifa, ili kuwezesha maamuzi sahihi na yenye tija katika usimamizi wa sera ya fedha na maendeleo ya uchumi wa nchi.

# BENKI KUU YAENZI WASTAAFU NA WAFANYAKAZI WALIOHUDUMU KWA MUDA MREFU




Naibu Gavana, Bw. Julian Banzi Raphael, akizungumza katika hafla ya kuwapongeza wastaafu na wafanyakazi waliohudumu kwa muda mrefu, iliyofanyika tarehe 25 Aprili 2025 BoT Dar es Salaam.

Benki Kuu ya Tanzania (BoT) imefanya hafla maalum ya kuwapongeza wastaafu na wafanyakazi waliohudumu kwa muda mrefu, iliyofanyika tarehe 25 Aprili 2025 katika ofisi ndogo za Makao Makuu jijini Dar es Salaam.

Akizungumza katika hafla hiyo, Naibu Gavana, Bw. Julian Banzi Raphael, aliwapongeza wafanyakazi hao kwa kujitoa kwao kwa hali na mali tangu wakiwa vijana hadi walipofikia hatua ya kustaafu. Alieleza kuwa utumishi wao wa muda mrefu umeonesha kiwango cha juu cha uvumilivu, uadilifu na kujituma ambavyo vimeiwezesha Benki Kuu kufikia mafanikio makubwa iliyonayo leo.

"Kitendo cha wafanyakazi kukaa Benki kwa kipindi kirefu hadi kustaafu ni ishara kwamba Benki Kuu ni mwajiri mzuri, anayejali ustawi wa wafanyakazi wake pamoja na familia zao," alisema Naibu Gavana Raphael. Aliongeza kuwa Benki Kuu siyo tu hutoa mishahara inayoridhisha, bali pia huwajengea wafanyakazi wake mazingira mazuri ya kujiendeleza kitaaluma na kimaisha.

Katika hotuba yake, Naibu Gavana alisisitiza kuwa Benki Kuu itaendelea kuwa mwajiri wa mfano na kuhakikisha inaendeleza utamaduni wa kuwatunza na kuwaendeleza wafanyakazi wake. Aidha, aliwahimiza wafanyakazi waliopo kuiga mfano wa wastaafu hao kwa kufanya kazi kwa bidii, uadilifu na kujitoa kwa taasisi yao.

Kwa upande mwingine, wastaafu waliagizwa kuendelea kuwa mabalozi wa Benki Kuu popote watakapokuwa, huku wakikumbushwa kuwa, "Once a Central Banker, always a Central Banker," akimaanisha kuwa utambulisho wao kama sehemu ya Benki Kuu utaendelea hata baada ya kustaafu.

Benki Kuu pia iliwahakikishia wastaafu kuwa itaendelea kuwapatia huduma muhimu, ikiwemo huduma za matibabu, kama sehemu ya kutambua mchango wao mkubwa walioutoa kipindi cha utumishi wao.

Hafla hiyo iliambatana na pongezi, zawadi na furaha kwa wastaafu waliotumikia taasisi hiyo kwa miaka mingi kwa uaminifu na kujituma, ikiashiria heshima kubwa wanayopewa na Benki Kuu ya Tanzania.



Naibu Gavana, Bw. Julian Banzi Raphael, akizungumza katika hafla ya kuwapongeza wastaafu na wafanyakazi waliohudumu kwa muda mrefu, iliyofanyika tarehe 25 Aprili 2025 BoT Dar es Salaam.



# GAVANA TUTUBA ASHIRIKI MIKUTANO YA IMF

Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Bw. Emmanuel Tutuba, ameshiriki kikao kati ya ujumbe wa Tanzania ulioongozwa na Waziri wa Fedha, Mhe. Dkt. Mwigulu Nchemba, na Mkurugenzi Mtendaji wa Kundi la Kwanza la Nchi za Afrika wa Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF), Bw. Adran Ubisse. Kikao hicho kililenga kujadili masuala ya kiuchumi pamoja na athari za mabadiliko ya sera za Marekani dhidi ya nchi za Afrika.

Dkt. Nchemba alieleza kuwa Tanzania imejipanga kukabiliana na athari za kusitishwa kwa misaada kutoka Marekani kwa kutegemea rasilimali za ndani kupitia Bajeti Kuu ya Serikali ya mwaka wa fedha 2025/2026.

Alibainisha kuwa Serikali imejipanga kubana matumizi ya kawaida na kuelekeza fedha zaidi kwenye huduma muhimu za jamii pamoja na sekta za uzalishaji, kwa lengo la kulinda uchumi wa taifa na kuhakikisha wananchi wanaendelea kupata huduma muhimu bila kutegemea misaada ya nje.

Mazungumzo hayo yamefanyika kando ya Mikutano ya Majira ya Kipupwe ya IMF na Benki ya Dunia, inayoendelea jijini Washington D.C., Marekani.





# GAVANA BOT, RAIS KAMPUNI YA VISA WAKUTANA WASHINGTON D.C



**Gavana Emmanuel Tutuba na Rais wa Kampuni ya VISA anayesimamia Ukanda wa Ulaya ya Kati, Mashariki ya Kati na Afrika, Bw. Andrew Torre, walipokutana katika Mikutano ya Majira ya Kipupwe ya IMF na Benki ya Dunia, iliyofanyika jijini Washington D.C., Marekani.**





Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Bw. Emmanuel Tutuba, amekutana na kufanya mazungumzo na Rais wa Kampuni ya VISA anayesimamia Ukanda wa Ulaya ya Kati, Mashariki ya Kati na Afrika, Bw. Andrew Torre.

Katika kikao hicho, viongozi hao walijadili kwa kina namna mbalimbali za kupunguza gharama za miamala ya kifedha, kudhibiti uhalifu wa kimtandao, na kuimarisha utoaji wa elimu ya fedha kwa wananchi. Masuala hayo yanalenga kupunguza matumizi ya fedha taslimu pamoja na kuongeza upatikanaji na matumizi ya huduma rasmi za kifedha, hasa zile zinazotolewa kwa njia ya kidigitali.

Aidha, kampuni ya VISA ilieleza dhamira yake ya kuendelea kushirikiana na Benki Kuu ya Tanzania kwa kutoa mafunzo na kubadilishana ujuzi wa kitaalamu, ili kuimarisha mifumo ya malipo kuwa salama, rahisi na jumuishi kwa Watanzania wote.

Kikao hicho pia kilihudhuriwa na Naibu Gavana, Dkt. Yamungu Kayandabila, Mkurugenzi wa Utafiti na Sera za Uchumi BoT, Dkt. Suleiman Missango, Meneja wa Sera ya Fedha BoT, Bi. Asimwe Bashagi, pamoja na maafisa waandamizi kutoka kampuni ya VISA.

Mazungumzo hayo yamefanyika sambamba na Mikutano ya Majira ya Kipupwe ya IMF na Benki ya Dunia, inayoendelea jijini Washington D.C., Marekani.

# BoT, IFC WAJADILI UPATIKANAJI WA MITAJI NA MIKOPO KWA SEKTA BINAFSI





Makamu wa Rais wa Taasisi ya Fedha ya Kimataifa ya Benki ya Dunia (IFC), Bw. John Gandolfo, akizungumza katika kikao na Gavana wa BOT,Bw. Emmanuel Tutuba kilichofanyika kwenye ukumbi wa mikutano wa Ubalozi wa Tanzania, jijini Washington D.C., Marekani.

Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Bw. Emmanuel Tutuba, amekutana na kufanya mazungumzo na Makamu wa Rais wa Taasisi ya Fedha ya Kimataifa ya Benki ya Dunia (IFC), Bw. John Gandolfo, katika ukumbi wa mikutano wa Ubalozi wa Tanzania, jijini Washington D.C., Marekani. Katika mazungumzo hayo, walijadili masuala mbalimbali yanayohusu namna ya kuongeza upatikanaji wa mitaji na mikopo kwa sekta binafsi, ufanisi na maendeleo ya masoko ya fedha na mitaji, pamoja na fursa za uwekezaji nchini Tanzania.

Gavana Tutuba alieleza kuwa uchumi wa Tanzania ni imara na thabiti, jambo linalodhihirishwa na viashiria mbalimbali vya kiuchumi. Alitoa wito kwa IFC pamoja na mashirika mengine ya kimataifa kuwawezesha kifedha wawekezaji wote wenye nia ya kuwekeza nchini Tanzania.

Kikao hicho pia kilihudhuriwa na Naibu Gavana, Dkt. Yamungu Kayandabila, Mkurugenzi wa Utafiti na Sera za Uchumi BoT, Dkt. Suleiman Missango, Meneja wa Sera ya Fedha BoT, Bi. Asimwe Bashagi, pamoja na maafisa waandamizi kutoka IFC.



# BOT YASHIRIKI MKUTANO WA AFREXIMBANK, ABUJA




Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Bw. Emmanuel Tutuba, ameshiriki katika Mkutano wa 32 wa Mwaka wa Benki ya Maendeleo ya Uagizaji na Uuzaji wa Bidhaa Afrika (Afreximbank), uliofanyika mjini Abuja, Nigeria kuanzia tarehe 25 hadi 28 Juni 2025.

Mkutano huo wa kimataifa ulijadili masuala mbalimbali ya kiutendaji na kimkakati ya benki hiyo, ukiwa umebeba kaulimbiu: "Kujenga Mwelekeo katika Miongo ya Ustahimilivu". Kaulimbiu hii ililenga kutathmini mafanikio yaliyopatikana kwa ustahimilivu wa taasisi hiyo na kujenga msingi imara wa maendeleo ya baadaye barani Afrika.

Katika mkutano huo, Gavana Tutuba alipata fursa ya kuchangia mada kuhusu "Uimara wa Taasisi za Kifedha kwa Maendeleo Endelevu ya Afrika na Umuhimu wa Hadhi Maalumu ya Mkopeshaji katika Kuwezesha Utafutaji wa Fedha kwa Ukuaji wa Afrika."

Akiwasilisha mada hiyo, Gavana Tutuba alisisitiza umuhimu wa kulinda hadhi hii maalumu kwa benki za maendeleo barani Afrika, ili ziendelee kuwa na uwezo wa kupata fedha kwa ajili ya kufadhili miradi mikubwa ya kimkakati.

Alitolea mfano wa Tanzania katika utekelezaji wa mradi wa reli ya kisasa ya SGR, ambapo Afreximbank kwa kushirikiana na taasisi nyingine, walishiriki kikamilifu katika kuwezesha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya mradi huo pamoja na Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere (JNHPP).




Katika hatua nyingine, Gavana Tutuba aliungana na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Philip Mpango, kutembelea Kituo cha Umahiri cha Matibabu ya Kibingwa cha Afrika kilichopo Abuja.

Kituo hicho ambacho kimefadhiliwa na Benki ya Afrexim kimewekwa miundombinu na vifaa tiba vya kisasa kwaajili ya matibabu ya kibingwa kukabiliana na maradhi mbalimbali ikiwemo saratani.

Aidha, Gavana Tutuba alipata nafasi ya kufanya mazungumzo na mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi na Rais wa Benki ya Afrexim Prof. Benedict Oramah, kando ya mkutano huo, kuhusu masuala mbalimbali ya ushirikiano kati ya Benki Kuu ya Tanzania na Afreximbank.



**Gavana Emmanuel Tutuba (wa tatu kutoka kulia) katika mjadala uliohusu Uimara wa Taasisi za Kifedha kwa Maendeleo Endelevu ya Afrika wakati Mkutano wa 32 wa Mwaka wa Benki ya Afreximbank uliofanyika mjini Abuja, Nigeria.**

# DKT. KAYANDABILA: WACHIMBAJI WADOGO WANAHITAJI MIFUMO RAFIKI YA MITAJI



**Naibu Gavana, Dkt. Yamungu Kayandabila, akizungumza katika mkutano wa wadau wa sekta ya madini uliofanyika tarehe 22 Mei 2025 jijini Dar es Salaam.**



**Naibu Gavana, Dkt. Yamungu Kayandabila, akizungumza katika mkutano wa wadau wa sekta ya madini uliofanyika tarehe 22 Mei 2025 katika hoteli ya Hyatt Regency jijini Dar es Salaam, ulioandaliwa na Benki ya Maendeleo ya Uuzaji wa Bidhaa Nje ya Afrika (Afreximbank) kwa kushirikiana na BoT.**




**Mkurugenzi Mtendaji wa Mahusiano na Wateja wa Afreximbank, Bw. Eric Monchu Intong, akielezea jambo katika mkutano wa wadau wa sekta ya madini uliofanyika tarehe 22 Mei 2025 jijini Dar es Salaam.**

Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Dkt. Yamungu Kayandabila, ametoa wito kwa taasisi za fedha na wadau wa sekta ya madini kubuni mifumo ya kifedha itakayowezesha wachimbaji wadogo na wa kati kupata mitaji kwa urahisi, ili kukuza sekta hiyo muhimu kwa uchumi wa nchi.

Akizungumza katika mkutano wa wadau wa sekta ya madini uliofanyika tarehe 22 Mei 2025 katika hoteli ya Hyatt Regency jijini Dar es Salaam, ulioandaliwa na Benki ya Maendeleo ya Uuzaji wa Bidhaa Nje ya Afrika (Afreximbank) kwa kushirikiana na BoT, Dkt.Kayandabila, alisema kuwa licha ya dhahabu kuchangia zaidi ya asilimia 90 ya mauzo ya madini nje ya nchi, wachimbaji wadogo bado wanakabiliwa na changamoto kubwa za kifedha zinazowazuia kukuza shughuli zao.

"Changamoto hizi zinatokana na uendeshaji usio rasmi, ukosefu wa kumbukumbu za kifedha, pamoja na hatari kubwa za kijiolojia katika miradi ya uchimbaji. Hii huwafanya wawe wa hatari kwa taasisi za kifedha," alisema Dkt. Kayandabila.

Alieleza kuwa taasisi nyingi za kifedha huona miradi ya wachimbaji wadogo kama miradi chipukizi isiyo na rekodi ya nyuma ya uendeshaji au nyaraka rasmi za kuaminika, hali inayosababisha hata miradi iliyokwisha kuanza na inayoonyesha mafanikio kushindwa kupata mikopo.

"Wachimbaji wengi wadogo wanashindwa pia kukidhi masharti ya dhamana au kufikia viwango vya uwazi wa taarifa vinavyotakiwa, jambo ambalo linawanyima fursa za kifedha," aliongeza.

Dkt. Kayandabila aliipongeza Afreximbank kwa ubunifu wao wa kifedha, akisema taasisi hiyo ina nafasi muhimu ya kujaza pengo lililoachwa na benki za biashara kwa kutoa mikopo ya mradi, dhamana za mikopo, na mbinu mbadala za utoaji wa mitaji.

Naye, Mkurugenzi Mtendaji wa Mahusiano na Wateja wa Afreximbank, Bw. Eric Monchu Intong, alisisitiza dhamira ya benki hiyo katika kuiwezesha sekta ya madini kupitia mkakati wa njia mbili: kuboresha upatikanaji wa fedha kwa ajili ya ununuzi wa vifaa vya uchimbaji na kusaidia ujenzi wa uwezo wa ndani.

Alisisitiza umuhimu wa kuongeza thamani kabla ya kuuza madini nje ya nchi, kama vile uchenjuaji wa madini hapa nchini, akisema hatua hiyo itaongeza ajira, kupunguza umasikini, na kuleta manufaa ya kiuchumi ya kudumu.

# GAVANA TUTUBA AHIMIZA MATUMIZI ZAIDI YA RASILIMALI ZA NDANI YA UKANDA WA EAC




Gavana Emmanuel Tutuba akikabidhiwa Mpango Mkuu wa Mfumo wa Malipo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Gavana wa Benki Kuu ya Kenya, Dkt. Kamau Thugge, katika Mkutano wa 28 wa Kamati ya Masuala ya Fedha (MAC) ya EAC uliofanyika tarehe 09 Mei 2025 jijini Mombasa, Kenya.

Benki kuu katika ukanda wa Afrika Mashariki (EAC) zimehimizwa kuweka kipaumbele katika kutumia rasilimali zao kwa ajili ya maendeleo yao, na kupunguza utegemezi kutoka nje.

Wito huo umetolewa na Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania, Bw. Emmanuel Tutuba, katika Mkutano wa 28 wa Kamati ya Masuala ya Fedha (MAC) ya Jumuiya ya Afrika Mashariki jijini Mombasa, Kenya.

Amesema nchi wanachama wa jumuiya hii zimebarikiwa kuwa na rasilimali nyingi zinazofaa kutumiwa kwa maendeleo ya kanda hii. Ameeleza kuwa licha ya maendeleo ambayo yamepatikana katika kipindi cha mwaka mmoja uliopita, ukanda wa Afrika Mashariki unaendeleo kupitia changamoto nyingi za kiuchumi.

"Kumekuwa na kuongezeka kwa ushuru katika biashara, migogoro ya kimataifa na athari zinazotokana na tabianchi ambavyo vinahatarisha utulivu wa kiuchumi na jitihada za mtangamo." Amesema Gavana Tutuba.

Aidha, ametaja kukua kwa huduma bunifu za kifedha (fintechs) na fedha za kidigitali (cryptocurrencies), kama maeneo ambayo licha ya kuweza kuchangia kukua na ufanisi wa ujumuishi wa kifedha, yanaleta changamoto za usimamizi na uhalifu wa kimtandao.

"Hivyo, ushirikiano wa pamoja katika kuhakikisha uthabiti wa kifedha pamoja na kusaidia ukuaji wa endelevu wa kiuchumi ni muhimu. Lazima tushirikishane njia bora za utendaji, data, na uzoefu kwa jinsi tunavyofanya kazi pamoja na kujenga mazingira bora kwa kuchangia kukuza uchumi, ubunifu na uthabiti kikanda." Alisema.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti katika kikao hicho, Magavana na wawakilishi kutoka Burundi, Rwanda, Somalia, Kenya, Sudani ya Kusini, Tanzania na Uganda, walielezea maendeleo ya kiuchumi ya nchi zao, pamoja na utayari wao wa kuhakikisha masuala ya mtangamano katika sekta kifedha yanafanikiwa.

Mkutano huo, ulioanza Jumatano na kamati ya wataalamu, umehitimishwa leo na magavana chini ya uenyekiti wa Gavana wa Benki Kuu ya Kenya, Dkt. Kamau Thugge. Aidha, viongozi hao wa benki kuu walitia saini taarifa ya pamoja ya mkutano huo inayoelezea yale yaliyojadiliwa na kukubaliwa katika mkutano huo.





Kutoka kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji, Utafiti na Uchambuzi wa Kiuchumi, akimwakilisha Gavana wa Benki Kuu ya Uganda Dkt. Adam Mugume; Gavana, Benki Kuu ya Tanzania, Bw. Emmanuel Tutuba; Gavana, Benki Kuu ya Sudan Kusini, Bw. Johnny Ohisa Damian; Gavana, Benki Kuu ya Kenya, Dkt. Kamau Thugge; Naibu Gavana, Benki Kuu ya Somalia, Dkt. Ali Yassin Sheikh; Gavana, Benki Kuu ya Rwanda, Bi. Soraya Hakuziyaremye; Gavana, Benki ya Jamhuri ya Burundi, Bw. Edouard Normand Bigendako; Naibu Katibu Mkuu (Forodha, Biashara na Masuala ya Fedha), Sekretarieti ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Bi. Annette Mutaawe Ssemuwemba.

# NAIBU GAVANA MSEMO: SERIKALI ZIHAMASISHE VYANZO MBADALA VYA FEDHA



Naibu Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Bi. Sauda Msemo, amezitaka serikali za Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara kuimarisha ukusanyaji wa rasilimali za ndani ili kupunguza utegemezi mkubwa kwa misaada ya kigeni inayopungua.

Akizungumza tarehe 28 Aprili 2025 katika mjadala ulioandaliwa na Shirika la Fedha Duniani (IMF) jijini Dar es Salaam, wakati wa uzinduzi wa Ripoti ya Uchumi wa Kanda ya Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara 2025, Bi. Msemo alisema kuna umuhimu wa kupanua wigo wa vyanzo vya fedha kwa kutafuta washirika wapya na mbinu mbadala za kupata fedha.

"Serikali zetu zinapaswa kujitahidi kuongeza mapato ya ndani na kupunguza utegemezi wa misaada kutoka mataifa ya nje. Pia, tunapaswa kutafuta vyanzo vipya vya mapato ili kuimarisha uwezo wetu wa kifedha," alisema.

Bi. Msemo alielezea kuwa mabadiliko ya ghafla katika sera za misaada za Marekani, yakiwemo kuondolewa kwa misaada katika sekta muhimu kama elimu, afya na miundombinu, yameleta changamoto kubwa kwa nchi nyingi Kusini mwa Jangwa la Sahara.

"Hatua za haraka zilizochukuliwa ni pamoja na kuongeza mgao wa bajeti kwa ajili ya kuendelea na utekelezaji wa programu muhimu, huku bajeti za miaka ijayo zikizingatia uendelevu wa miradi katika sekta hizo muhimu." Alisema.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Stanbic nchini, Bw. Manzi Rwegasira, alisema ili sekta binafsi ivutie uwekezaji, ni muhimu kwa serikali kuimarisha mazingira ya biashara kwa kuboresha mifumo ya kodi, kutoa dhamana kwa mikopo na kushirikiana katika uwekezaji kwenye miradi.

Naye, Naibu Mkurugenzi wa IMF Idara ya Afrika, Bi. Cathy Pattillo, alisema nchi nyingi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara zina uwezo wa kuongeza mapato ya ndani, lakini kiwango cha ukusanyaji kodi kwa sasa bado kiko chini ya matarajio ukilinganisha na uwezo uliopo. Alisisitiza kuwa mapato ya ndani ni chanzo cha uhakika na endelevu cha maendeleo.

Mwakilishi wa IMF nchini, Bw. Sebastian Acevedo, amesisitiza umuhimu wa kuwa watumishi wenye ujuzi wa kutosha ili kuweza kufaidika na idadi kubwa ya watu barani Afrika ili kukabili changamoto mbalimbali za kiuchumi zinazoibuka.



**Naibu Gavana, Bi. Sauda Msemo (katikati), akifafanua jambo katika mjadala ulioandaliwa na Shirika la Fedha Duniani (IMF) jijini Dar es Salaam, tarehe 28 Aprili 2025.**



**Wageni waalikwa wakifwatilia mjadala ulioandaliwa na Shirika la Fedha Duniani (IMF) jijini Dar es Salaam, tarehe 28 Aprili 2025.**

# GAVANA NA BALOZI WAKUTANA KUJADILI USHIRIKIANO WA KIUCHUMI



Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Bw. Emmanuel Tutuba, na Balozi wa Uingereza nchini Tanzania, Mhe. Marianne Young, walipokutana katika ofisi za Benki Kuu jijini Dar es Salaam tarehe 29 Aprili 2025.

Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Bw. Emmanuel Tutuba, amekutana na kufanya mazungumzo na Balozi wa Uingereza nchini Tanzania, Mhe. Marianne Young, katika ofisi za Benki Kuu jijini Dar es Salaam tarehe 29 Aprili 2025.

Katika mazungumzo hayo, Gavana Tutuba alieleza kuwa uchumi wa Tanzania umeendelea kuimarika licha ya changamoto mbalimbali za kiuchumi duniani. Alibainisha kuwa kwa kipindi kinachoishia Desemba 2024, uchumi wa Tanzania ulikua kwa asilimia 5.5, hali inayoonesha ustahimilivu wa kiuchumi wa taifa.

Aidha, Gavana Tutuba alifafanua kuwa kuimarika kwa uchumi kumeambatana na kudhibitiwa kwa mfumuko wa bei, ambao ulikuwa asilimia 3.1 kufikia Desemba 2024.

Aliongeza kuwa sekta ya fedha nchini inaendelea kukua kwa kasi, huku Benki Kuu ikiimarisha juhudi za kuongeza huduma jumuishi za fedha kwa wananchi wote, ili kuhakikisha Watanzania wengi zaidi wanatumia mifumo rasmi ya fedha na kuchangia maendeleo ya taifa.

Kwa upande wake, Balozi Young alipongeza juhudi za Benki Kuu katika kusimamia uchumi wa nchi. Alisisitiza kuwa Uingereza itaendelea kushirikiana na BoT katika masuala ya uchumi na fedha, sambamba na kukuza maendeleo endelevu ya Tanzania.

Miongoni mwa waliohudhuria kikao hicho ni Naibu Gavana wa Sera za Uchumi na Fedha, Dkt. Yamungu Kayandabila, Naibu Gavana wa Uthabiti na Usimamizi wa Sekta ya Fedha, Bi. Sauda Msemo, pamoja na maafisa waandamizi kutoka menejimenti ya Benki Kuu ya Tanzania.



Naibu Gavana, Sera za Uchumi na Fedha, Dkt. Yamungu Kayandabila, akizungumza katika kikao kati ya BoT na Balozi wa Uingereza nchini Tanzania.








# BENKI KUU: WATALII KURUHUSIWA KULIPA KWA FEDHA ZA KIGENI

Benki Kuu ya Tanzania imetoa ufafanuzi kuhusu Kanuni za Matumizi ya Fedha za Kigeni za Mwaka 2025, ikieleza kuwa malipo ya bidhaa na huduma kati ya wakazi na wageni, wakiwemo watalii, yanaweza kufanyika kwa kutumia fedha za kigeni.

Akizungumza katika mjadala uliofanyika kwenye Maonesho ya Karibu Kili-fair jijini Arusha tarehe 8 Juni 2025, Mkurugenzi wa Masoko ya Fedha wa Benki Kuu ya Tanzania, Bw. Emmanuel Akaro, alifafanua kuwa hatua hiyo inalenga kuwezesha mazingira rafiki ya kibiashara kwa wageni na urahisi wa miamala katika sekta ya utalii.

"Mawakala wa utalii ambao ni wakazi, wanaruhusiwa kutumia fedha za kigeni kulipia huduma mbalimbali zinazotolewa kwa watalii kutoka nje ya nchi,"alisema.

Alisisitiza kuwa malipo yote kati ya wakazi lazima yafanyike kwa Shilingi ya Tanzania, na ni kosa kwa mtoa huduma yeyote kukataa malipo yanayofanyika hapa nchini kwa kutumia Shilingi ya Tanzania.

Bw. Akaro aliongeza kuwa Kanuni hizi zimetungwa ili kutekeleza Kifungu cha 26 cha Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania ya mwaka 2006, na zimeanza kutumika rasmi kuanzia tarehe 28 Machi 2025.

"Tangu kuanza kutumika kwa kanuni hizo, kumekuwa na matokeo chanya ikiwemo kuongezeka kwa ukwasi wa fedha za kigeni. Kwa mfano, miamala ya Dola za Marekani kwenye soko la fedha za kigeni la rejareja nchini imeongezeka kutoka wastani wa dola milioni 40 hadi milioni 69 kwa siku", alisema.



**Mkurugenzi wa Masoko ya Fedha, Bw. Emmanuel Akaro, akizungumza katika mjadala kuhusu Kanuni za Matumizi ya Fedha za Kigeni za Mwaka 2025, uliofanyika kwenye Maonesho ya Karibu-Kilifair jijini Arusha tarehe 8 Juni 2025.**

Vilevile, alibainisha kuwa, kutokana na kuongezeka kwa ukwasi wa fedha za kigeni, thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola ya Marekani imeimarika kwa kiwango kikubwa, na matarajio ni kwamba itaendelea kuimarika zaidi.

"Hii ni kutokana na kuanza kwa msimu wa mapato ya fedha za kigeni, hususan kutoka kwenye sekta kama utalii, kilimo na mauzo ya bidhaa nje ya nchi, ambazo kwa kawaida huingiza fedha nyingi za kigeni katika kipindi hiki,"alisema.

Benki Kuu ya Tanzania inaendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu utekelezaji wa kanuni hizi, ili kuhakikisha kwamba zinazingatiwa kwa manufaa ya uchumi wa taifa na ustawi wa sekta za kibiashara, hasa utalii.


Tajiri kwa sababu ni wewe, kodi nitakufanyia USD 1000 tu kwa mwezi.
DALALI KASONGO
Kwa taarifa yako, tangu tarehe 28 Machi 2025 ni kosa kupanga bei kwa kutumia fedha za kigeni. Weka bei yako kwa Shilingi tafadhali.
SHILINGI YETU UCHUMI WETU
Kama unavyoona tajiri, nyumba hii ni ya kisasa kabisa. Kodi ni USD 1,200 kwa mwezi.
Sikia Kasongo! Hatupo Marekani bwana, hapa ni Tanzania, bei zote zinatakiwa kuwa kwa Shilingi yetu.
Unachofanya ni kinyume na Kanuni za Matumizi ya Fedha za Kigeni za Mwaka 2025.
NYUMBA INAPANGISHWA
Bei na malipo ya bidhaa na huduma zote ndani ya nchi zinapaswa kufanyika kwa Shilingi ya Tanzania.

# SERIKALI YASISITIZA MATUMIZI YA SHILINGI KATIKA MALIPO NDANI YA NCHI

Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania (BoT) imetoa wito kwa wadau wa sekta ya utalii na wananchi kwa ujumla kuhakikisha kuwa malipo ya bidhaa na huduma zote ndani ya nchi yanafanyika kwa Shilingi ya Tanzania, kama ilivyoainishwa katika Kanuni za Matumizi ya Fedha za Kigeni za Mwaka 2025.
Wito huo umetolewa na Meneja wa Idara ya Uchumi wa Kimataifa na Sekta za Uzalishaji kutoka BoT, Bi. Villela Waane, katika semina ya wadau wa utalii iliyoandaliwa na Wizara ya Maliasili na Utalii, na kuongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Mhe. Dkt. Hassan Abbas, jijini Dodoma tarehe 28 Mei 2025.

Bi. Waane alieleza kuwa Kanuni hizo zilizochapishwa katika Gazeti la Serikali Na. 198 la tarehe 28 Machi 2025, zinatekelezwa kwa mujibu wa Kifungu cha 26 cha Sheria ya Benki Kuu ya mwaka 2006. Alisisitiza kuwa ni kosa la kisheria kunukuu au kutangaza bei kwa fedha za kigeni, au kupokea malipo kwa fedha hizo ndani ya nchi.

"Matumizi ya Shilingi ni muhimu kwa utekelezaji wa sera ya fedha, udhibiti wa mfumuko wa bei, na ustawi wa uchumi wa taifa. Shilingi ni ishara ya utaifa na utambulisho wetu," alisema Bi. Waane.

Naye, Mkurugenzi wa Masoko ya Fedha, Bw. Emmanuel Akaro, aliongeza kuwa Kanuni mpya zinaruhusu miamala michache tu kufanyika kwa fedha za kigeni. Mikataba ya malipo kwa fedha za kigeni haitaruhusiwa kuanzishwa wala kuhuishwa kuanzia tarehe 28 Machi 2025. Watalii na wageni kutoka nje ya nchi wanapaswa kubadilisha fedha kupitia benki au maduka rasmi ya kubadilisha fedha, au kutumia njia za kidigitali kama kadi.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Dkt. Hassan Abbas, aliwataka wadau kushirikiana na Serikali kutekeleza Kanuni hizo zenye lengo la kusaidia kuimarisha uchumi, kulinda thamani ya Shilingi ya Tanzania, na kuleta utulivu wa kifedha nchini.

Ushiriki wa BoT katika semina hiyo ni sehemu ya juhudi za kutoa elimu kwa wadau wa sekta mbalimbali nchini ili kuwaongezea uelewa kuhusu utekelezaji wa Kanuni za Matumizi ya Fedha za Kigeni za Mwaka 2025, pamoja na umuhimu wa kutumia Shilingi ya Tanzania katika miamala yote ya ndani ya nchi.





Meneja Idara ya Uchumi wa Kimataifa na Sekta za Uzalishaji kutoka BoT, Bi. Villela Waane, akifafanua jambo kuhusu Kanuni za Matumizi ya Fedha za Kigeni katika semina ya wadau wa sekta ya utalii.



Katibu Mkuu wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Dkt. Hassan Abbas, akizungumza katika semina ya wadau wa sekta ya utali.



Mwenyekiti wa Chama cha Mawakala wa Utalii Tanzania (TATO), Bw. Wilbard Chambulo, akielezea jambo kuhusu sekta ya utalii katika semina ya wadau wa sekta ya utalii.



Mkurugenzi wa Masoko ya Fedha, Bw. Emmanuel Akaro, akifafanua jambo kuhusu Kanuni za Matumizi ya Fedha za Kigeni katika semina ya wadau wa sekta ya utali.

# MABENKI YATAKIWA KUIMARISHA USIMAMIZI WA VIHATARISHI VYA MIKOPO, KUDUMISHA UADILIFU

Wadau wa sekta ya fedha nchini wametakiwa kuimarisha mbinu zao za usimamizi wa vihatarishi vya mikopo na kuhakikisha uadilifu katika utekelezaji wa shughuli zao za kila siku ili kulinda uthabiti wa mfumo wa fedha na kusaidia utoaji wa mikopo kwa njia salama na endelevu katika taasisi zao.



Wito huo umetolewa na Mkurugenzi wa Usimamizi wa Sekta ya Fedha, Benki Kuu ya Tanzania (BoT) Bw. Sadati Musa (pichani kulia) wakati wa ufunguzi rasmi wa warsha kuhusu usimamizi wa vihatarishi vya mikopo kwa maofisa wa mikopo kutoka mabenki na taasisi mbalimbali za kifedha.

Bw. Sadati amepongeza juhudi za sekta hiyo katika kuboresha usimamizi wa hatari za mikopo, na kueleza kuwa kiwango cha mikopo chechefu (NPLs) kimeshuka kutoka asilimia 9.42 mwaka 2020 hadi asilimia 3.43 kufikia Mei 2025.

Hata hivyo, amesisitiza kuwa bado kuna kazi ya ziada inayopaswa kufanywa na kila benki katika kuboresha mifumo yao ya udhibiti wa ndani na usimamizi wa vihatarishi.

Bw. Sadati ameelezea umuhimu wa kuwajengea wafanyakazi wa benki uwezo na kuwapa nyenzo sahihi za kupunguza hatari hizo kwa ufanisi huku akiwataka washiriki kutumia fursa hiyo kushiriki kikamilifu katika mijadala na kubadilishana uzoefu kwa vitendo ili kuimarisha uwezo wa pamoja wa sekta.

Warsha hiyo inayofanyika katika Ofisi za Makao Makuu Ndogo ya Benki Kuu ya Tanzania jijini Dar es Salaam kuanzia tarehe 16 hadi 20 Juni 2025, inatarajiwa kujadili masuala mbalimbali yanayohusu usimamizi wa vihatarishi vya mikopo, yakiwemo masharti ya kisheria, usimamizi wa mali zenye hatari, kushughulikia mikopo chechefu, upangaji madaraja ya mikopo na uwekaji wa akiba, pamoja na matumizi ya mabaraza ya kumbukumbu za wakopaji.



# DIB YAFANIKISHA MALIPO YA ASILIMIA 55 KWA WADAI WA ILIYOKUWA BENKI YA FBME




**Mkurugenzi wa Bodi ya Bima ya Amana, Bw. Isack Kihwili, akitoa taarifa ya ulipaji fedha za iliyokuwa benki ya FBME.**

Bodi ya Bima ya Amana (DIB) imefanikisha upatikanaji wa malipo ya asilimia 55 kwa awamu mbili kwa wadai wa iliyokuwa benki ya FBME. Hao ni wale waliokuwa na fedha zaidi ya kiwango cha juu cha kinga kilichokuwa kinatumika wakati huo cha shilingi 1,500,000.

Akizungumzia mchakato wa ufilisi wa benki ya FBME, Mkurugenzi wa DIB, Bw. Isack Kihwili, anasema licha ya kulipa asilimia 55 kwa awamu mbili, mchakato huo wa ufilisi umekuwa na changamoto kutokana na utofauti wa sheria za ufilisi za Tanzania na Cyprus pamoja na kesi nyingi zilizojitokeza mara baada ya benki hiyo kufutiwa leseni.

Fedha zilizotolewa kwa awamu ya kwanza ni asilimia 30 sawa na TZS Milioni 10,563.89, wakati katika awamu ya pili ya asilimia 25 jumla ya pesa iliyopatikana ni TZS milioni 8,991.75.

Katika kiasi hicho, awamu ya kwanza jumla ya wateja 968 kati ya 1,414 wamelipwa fidia ya TZS Milioni 9,137.77, sawa na asilimia 86.5, huku awamu ya pili ya asilimia 25, wateja 960 kati ya jumla ya wateja 1,414 wamelipwa fidia ya jumla ya Shilingi Milioni 7,566.61 (sawa na asilimia 86.0 ya fedha iliyopatikana).

"Idadi ya wateja ambao hawajalipwa fidia ya ufilisi ya kiwango cha asilimia 30 kwa sababu mbalimbali hadi Mei 2025 ni 446, wenye jumla ya madai ya jumla ya TZS Milioni 1,425.14," ameeleza Bw. Kihwili.

Aidha, hadi mwezi Mei 2025, wateja 454 (sawa na asilimia 32) hawajalipwa fidia ya ufilisi ya kiwango cha asilimia 25 kwa sababu mbalimbali. Jumla ya madai yao ni Shilingi Milioni 1,235.81 (asilimia 14).
Bw. Kihwili amesema DIB itaendelea kufanya malipo kwa wadai kadiri makusanyo ya mali za benki hiyo yatakavyokuwa yanapatikana."

FBME Bank Limited (ambayo ipo chini ya ufilisi) ilianza rasmi kuendesha shughuli zake za biashara ya kibenki nchini Tanzania Juni 18, 2003. Makao Makuu ya benki hiyo yalikuwa Dar es Salaam, Tanzania na ilikuwa na tawi moja nchini Cyprus.

Kulingana na takwimu zilizopo, inakadiriwa kuwa zaidi ya asilimia 90 ya shughuli za benki hiyo zilikuwa nchini Cyprus, huku chini ya asilimia 10 zikiwa hapa Tanzania.

Hata hivyo, Benki Kuu ya Tanzania (BoT) pamoja na Benki Kuu ya Cyprus (CBC) zilifunga na kufuta leseni ya biashara ya FBME Bank Limited mnamo mwezi Mei 2017 baada ya benki hiyo kuthibitika kukiuka masharti ya leseni ya kuendesha biashara ya kibenki.

Baada ya Benki Kuu ya Tanzania kufuta leseni ya benki ya FBME, kwa mujibu wa mamlaka iliyonayo iliiteua DIB kuwa mfilisi.

Kuhusu kuchelewa kulipwa kwa fedha hizo, ikiwa ni pamoja na kulipwa kwa awamu, Bw. Kihwili anasema; "Pande zote mbili (DIB na Wakala wa ufilisi nchini Cyprus) tunaendelea kukusanya mali za FBME Bank Limited zilizopo nchini na nje ya nchi pamoja na kufuatilia uondolewaji wa vikwazo vilivyowekwa na mamlaka za Marekani (FinCEN) ili fedha ziweze kupatikana na kulipa wadai kwa awamu zinazofuata."

Wakati huohuo, Mkurugenzi wa DIB amesema ufilisi wa taasisi nyingine zilizofutiwa leseni ya biashara na Benki Kuu unaendelea vizuri na uko katika hatua mbalimbali za utekelezaji.

Alizitaja benki hizo kuwa ni Greenland Bank Tanzania Limited (iliyofungwa mwaka 2000) na Delphis Bank Tanzania Limited (iliyofutiwa leseni mwaka 2003), ambazo ufilisi wake uko katika hatua za mwisho.

"Malipo ya fidia ya ufilisi yanaendelea kwa benki za Njombe Community Bank Limited (2017), Kagera Farmers' Cooperative Bank Limited (2018), Mbinga Community Bank Plc (2018) na Meru Community Bank Limited (2018)," ameeleza Mkurugenzi wa DIB.

Bw. Kihwili amesema malipo yanafanywa na kuwataka waliokuwa wateja wa taasisi hizo ambao hawajalipwa fedha zao kuwasiliana na DIB kupitia ofisi zake zilizopo kwenye majengo ya Benki Kuu ya Tanzania Dodoma na Dar es Salaam ili mchakato wa malipo yao uweze kufanyika.

"Ulipaji wa fidia ya ufilisi kwa benki za Covenant Bank For Women (T) Limied (2018) na Efatha Bank Limited (2018) bado haujaanza. Wadai watataarifiwa pindi ulipaji utakapoanza," ameeleza.

# JAMII YAZIDI KUHAMASIKA MATUMIZI YA HUDUMA ZA FEDHA MTANDAO



Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) imeweka bayana kwamba idadi ya akaunti zinazotumia huduma za kifedha kupitia simu za mkononi imeendelea kuongezeka. Katika taarifa iliyochapishwa kwenye tovuti ya Mamlaka hiyo, idadi ya akaunti za miamala ya kifedha imeongezeka karibu mara mbili kati ya mwaka 2021 na Desemba 2024.

Taarifa hiyo inaeleza kuwa hadi Desemba 2024 akaunti zinazotumia huduma za kifedha kupitia simu za mkononi zilikuwa 61,882,499 kutoka 32,720,180 iliyorekodiwa Desemba 2021.

Katika kipindi hicho, kiwango cha kuongezeka usajili wa akaunti za pesa kwa simu za mkononi kilizidi kile cha usajili wa laini za simu jambo linaloonesha kwamba watumiaji wengi wa simu za mkononi wanajisajili kwa huduma za fedha mtandaoni na kidijiti, hivyo kuingia kwenye mfumo shirikishi wa kifedha.

Wakati laini za simu zilizosajiliwa ziliongezeka kwa asilimia 65.4 kati ya Machi 2021 na Desemba 2024, akaunti za fedha kwa simu ziliongezeka kwa wastani wa asilimia 89.1.

Vilevile malipo ya kielektroniki yanawezesha mamlaka zinazosimamia mapato kudhibiti mapato ya serikali na sekta ya umma, hasa baada ya serikali kuanzisha mfumo wa malipo ya kiserikali mtandaoni (GePG).

Benki Kuu ya Tanzania na TCRA zinashirikiana katika usimamizi wa huduma za fedha mtandaoni ambapo Benki Kuu ya Tanzania inasimamia sekta ya fedha kwa ujumla na kutoa leseni za huduma za fedha mitandaoni wakati TCRA inatoa leseni kwa watoa huduma za simu za mkononi na kuwapa namba za mawasiliano na misimbo, au namba fupi ya kuwezesha miamala hiyo.



# UMUHIMU WA KUFANYA MALIPO NA MIAMALA KIDIJITALI

**Katika dunia ya sasa ambayo teknolojia inakua kwa kasi, kufanya malipo na miamala kwa njia ya mtandao (kidijitali) kumeleta mapinduzi makubwa katika namna watu wanavyofanya shughuli zao za kifedha. Njia hizi zinahusisha matumizi ya mifumo ya benki mtandaoni, programu za simu (mobile money), kadi za kielektroniki, na huduma nyingine za malipo za kidijitali**

**Malipo ya kidijitali yameibuka kuwa njia salama, rahisi, na ya kisasa ya kufanya miamala. Benki Kuu ya Tanzania, ambayo ina jukumu la kuandaa na kusimamia utekelezaji wa sera ya fedha nchini, inahamasisha Watanzania kubadili mtazamo wa matumizi ya fedha taslimu na kuelekea kufanya malipo kidijitali.**

**Kufanya malipo kidijitali kuna faida lukuki. Zifuatazo ni sababu kuu zinazofanya malipo ya kidijitali kuwa ya muhimu:**

## Urahisi na uharaka

Malipo ya kidijitali yanafanyika kwa haraka bila hitaji la kusafiri hadi benki au ofisi fulani. Mtu anaweza kutuma au kupokea fedha popote alipo, muda wowote, kwa kubofya tu kwenye simu au kompyuta. Pengine una ndugu au rafiki anayehitaji msaada wa fedha kwa haraka, utaweza kumsaidia punde bila hata kunyanyuka mahali ulipo au pengine unahitaji kuagiza bidhaa au huduma fulani mfano chakula, unaweza kuagiza na kuomba kiandaliwe kabla haujafika ili utakapofika, usipoteze muda mwingi kusubiri kwa sababu tu ilibidi ufike, ulipie huduma au bidhaa ndipo ianze kuandaliwa.

Kufanya malipo kidijitali kunapunguza hatari ya kupoteza fedha taslimu au kuibiwa, kwani miamala hufanyika moja kwa moja kupitia kadi za benki au programu na mitandao ya simu. Teknolojia ya kisasa inahakikisha usalama wa hali ya juu, huku ikiwapa wateja uhakika wa usimamizi mzuri wa fedha zao kwani mifumo ya malipo ya kidijitali imewekewa ulinzi wa nambari za siri, alama za vidole, au uthibitisho wa hatua mbili (two-factor authentication).

## Ufuatiliaji na usimamizi bora wa fedha

Malipo ya kidijitali yanakuza uwazi na urahisi wa kufuatilia matumizi kwani huacha kumbukumbu ya kila malipo au mapokezi ya fedha, jambo linalorahisisha ufuatiliaji wa matumizi na kuweka bajeti kwa usahihi zaidi. Hili ni muhimu hasa katika kufikia malengo ya kifedha.




Kufanya malipo kidijitali kunapunguza changamoto za muda na gharama. Kwa kufanya miamala kidijitali, mtumiaji anaepukana na usumbufu wa kupanga foleni ndefu au kusumbuka kutumia muda mwingi kuhesabu fedha taslimu au kutumia gharama kusafiri kufuata huduma ambayo angeweza tu kufikishiwa baada ya kuilipia mtandaoni.

## Kuchochea maendeleo ya kiuchumi

Mfumo thabiti wa malipo ya kidijitali huchochea biashara mtandaoni (e-commerce), na kuwezesha watu wengi kujihusisha na biashara bila vizuizi vya kijiografia. Pia, fedha nyingi zinakuwa zikizunguka katika mifumo rasmi ambayo ni rahisi kufuatilia. Kwa kuwa miamala ya kidijitali inaacha rekodi, serikali inaweza kukusanya kodi kwa ufanisi zaidi kupitia mfumo wa kielektroniki, hivyo kuongeza mapato ya ndani kwa ajili ya maendeleo ya taifa.

## Kupunguza ufisadi na matumizi mabaya ya fedha

Kila muamala wa kidijitali huandikwa moja kwa moja kwenye mfumo wa kidijitali. Hii inamaanisha kuwa taasisi au mamlaka za fedha zinaweza kufuatilia kwa urahisi ni nani alipokea fedha, kiasi gani, lini, na kwa sababu ipi. Mara nyingi fedha taslimu hutumika katika vitendo vya kifisadi kwa sababu hakuna uthibitisho wa miamala. Kwa kupunguza matumizi ya pesa taslimu na kutumia mifumo ya kidijitali, inakuwa vigumu kwa mtu kuficha matumizi au kupokea "rushwa kwa siri". Hali hii huongeza uwazi na kuwafanya watumishi wa umma au viongozi wa taasisi kuwajibika zaidi kwa matumizi ya fedha za umma.

## Kuwasaidia Wafanyabiashara

Malipo ya kidijitali hurahisisha upokeaji wa fedha kwa wafanyabiashara, jambo linalowasaidia kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma. Pia, hupunguza hitaji la kuwa na fedha taslimu dukani, jambo linalosaidia katika usimamizi wa fedha na usalama.

## Ujumuishi wa Kifedha (Financial Inclusion)

Malipo ya mtandao yanatoa fursa kwa watu walioko maeneo ya mbali au wasio na akaunti za benki kupata huduma za kifedha kupitia simu zao, hivyo kupanua wigo wa huduma rasmi za kifedha kwa wananchi wengi zaidi.

Kutumia malipo ya kidijitali si tu kwamba kunarahisisha maisha ya kila siku, bali pia kuna mchango mkubwa katika kukuza uchumi wa taifa, kuimarisha uwajibikaji, na kuongeza usalama wa kifedha kwa mtu binafsi na jamii kwa ujumla. Jamii inahamasishwa kutumia zaidi teknolojia hii kifedha yenye usalama, urahisi, na manufaa makubwa kwa maisha ya kila siku na kwa mustakabali wa uchumi wa kisasa.

# NUNUA NA UZA VITU KWA KUTUMIA SHILINGI

Kanuni mpya tayari, matumizi ya Shilingi,
Ni sheria si hiyari, jambo hili la msingi,
Ukitii ni vizuri, usijekwaa kigingi,
Nunua na uza vitu, kwa kutumia Shilingi.

Kama unapanga bei, zote ziwe kwa Shilingi,
Kanuni haitetei, kukwepakwepa Shilingi,
Wala haikuchekei, ukiikwepa Shilingi,
Nunua na uza vitu, kwa kutumia Shilingi.

Hili utambue wazi, ukitumia Shilingi,
Wewe ni mtendakazi, kwenye uchumi msingi,
Kwa mchango huo wazi, jua waupiga mwingi,
Nunua na uza vitu, kwa kutumia Shilingi.

Ni kosa bei kupanga, nje ya yetu Shilingi,
Au bidhaa kupanga, kutouza kwa Shilingi,
Kanuni hizi za lenga, kuipa hadhi Shilingi,
Nunua na uza vitu, kwa kutumia Shilingi.

Ni makosa kunukuu, bei nje ya Shilingi,
Uache uchovu huu, kutoijali Shilingi,
Kutumia za majuu, usiseme hujipingi,
Nunua na uza vitu, kwa kutumia Shilingi.

Bei zako bainisha, kwa kutumia Shilingi,
Uache kulazimisha, za nje una Shilingi,
Hapo utasababisha, kuzorotesha Shilingi,
Nunua na uza vitu, kwa kutumia Shilingi.

Bidhaa tunalipia, kwa kutumia Shilingi,
Huduma twanunulia, kwa kutumia Shilingi,
Usijemkatalia, mtu na zake Shilingi,
Nunua na uza vitu, kwa kutumia Shilingi.

Wageni waje nchini, wajipatie Shilingi,
Si kwa fedha za kigeni, kwa huduma za msingi,
Vinginevyo ni uhuni, kutotumia Shilingi,
Nunua na uza vitu, kwa kutumia Shilingi.

Lakini kwa wenye kadi, hilo jambo la msingi,
Hizo zakidhi akidi, sawasawa na Shilingi,
Tena zafaa zaidi, hasa huo ni udingi,
Nunua na uza vitu, kwa kutumia Shilingi.

Kuzikiuka kanuni, kutotumia Shilingi,
Tajitia Msambweni, siseme hawakufungi,
Lakini yako amani, zidi tumia Shilingi,
Nunua na uza vitu, kwa kutumia Shilingi.

Sera ya Fedha ya nchi, yategemea Shilingi,
Hiyo iko kwenye nchi, hivyo jambo la msingi,
Tuhakiki hatuachi, kuitumia Shilingi,
Nunua na uza vitu, kwa kutumia Shilingi.

Hebu kipende chako, pesa yako ni Shilingi,
Na tena tumia chako, kwa malipo ni Shilingi,
Kokote kule uliko, uithamini Shilingi,
Nunua na uza vitu, kwa kutumia Shilingi.

**na Lwaga Mwambande.**

**Limetolewa na Idara ya Mawasiliano**
**Benki Kuu ya Tanzania**

---

Anuani:
**Barabara ya 16 ya Jakaya Kikwete, 40184**
**S.L.P. 2303 Dodoma, Tanzania**
Barua pepe:
**botcommunications@bot.go.tz**
**info@bot.go.tz**
Tovuti:
**www.bot.go.tz**